ذو القعدة من معاني الحجّ وأسراره .

بسم الله الرّحمن الرّحيم

الحَمدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ، جَعَلَ الْبَيْتَ الْحَرَامَ مِنْ أَعْظَمِ شَعَائِرِ الإِسْلاَمِ ، وَجَعَلَ الْحَجَّ كَفَّارَةً لِلْخِطَايَا وَالآثَامِ . أَحْمَدُهُ سُبْحَانَهُ بِمَا هُوَ لَهُ أَهْلٌ مِنَ الْحَمْدِ وَأُثْنِي عَلَيْهِ ، وَأَسْتَغْفِرُهُ مِنْ جَمِيعِ الذُّنُوبِ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ ، وَأُومِنُ بِهِ وَأَتَوَكَّلُ عَلَيهِ ، مَنْ يَهْدِهِ اللهُ فَلاَ مُضِلَّ لَهُ ، وَمَنْ يُضْلِلْ فَلاَ هَادِيَ لَهُ . وَأَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ ، شَهَادَةً تَقُودُ إِلَى دَارِ السَّلاَمِ . وَأَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ ، أَفْضَلُ نَبِيٍّ مُرْسَلٍ وَإِمَامُ كُلِّ نَاسِكٍ ، صَلَّى اللهُ عَلَيهِ وَسَلَّمَ وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ ، وَعَلَى كُلِّ مَنِ اهْتَدَى بِهَدْيِهِ وَاسْتَنَّ بِسُنَّتِهِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلاً سَدِيداً }الأحزاب70

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ }الحشر18

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ ، وَالْعَمَلِ بِمَا فِيْهِ رِضَاهُ ، فَاتَّقُوا اللهَ وَرَاقِبُوهُ ، وَامْتَثِلُوا أَوَامِرَهُ وَلاَ تَعْصُوهُ ، وَاذْكُرُوهُ وَلاَ تَنْسَوهُ ، وَاشْكُرُوهُ وَلاَ تَكْفُرُوهُ .

Enyi Waja wa ALLAH :

Hakika nyinyi mpo katika siku za maandalizi ya safari ya Hija, basi muitikieni Mola wenu mtukufu aliekuiteni kwenye nyumba yake ya kale na akakuongozeni kwenye nguzo ya imani.

Imepokewa kutoka kwa Ibnu Abbas (ra) ya kuwa amesema :

“ Alitukhutubia Mjumbe wa ALLAH (saw) akasema “ :

((يَا أَيُّهَا النَّاسُ كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْحَجُّ))

“ Enyi watu imefaradhishwa juu yenu Hija” , Akasimama Al-Aqrau bin Habis akauliza : “Jee katika kila mwaka ewe Mjumbe wa ALLAH ?”

Akasema Mtume (saw) :

((لَوْ قُلْتُهَا لَوَجَبَتْ ، وَلَوْ وَجَبَتْ لَمْ تَعْمَلُوا بِهَا وَلَمْ تَسْتَطِيْعُوا ، اَلْحَجُّ مَرَّةً ، فَمَنْ زَادَ فَهُوَ تَطَوَّعٌ))

“ Ningesema hivyo ingekuwa wajibu, na kama ingewajibika musingeifanya wala musingeiweza, hija ni mara moja tu, na atakaezidisha huwa ni ibada ya khiari”.

Na anasema ALLAH (SW) :

{وَلِلّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلاً وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ الله غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ } آل عمران97

“ Na ALLAH amewawajibishia watu wafanye hija katika nyumba hiyo, kwa yule awezae kufunga safari ya kwenda huko, na atakekanusha basi ALLAH si muhitaji kwa walimwengu”.

Na imepokewa ya kuwa Mtume (saw) amesema :

((تَابِعُوا بَيْنَ الْحَجِّ وَالْعُمْرَةِ فَإِنَّهُمَا يَنْفِيَانِ الْفَقْرَ وَالذُّنُوبَ كَمَا يَنْفِي الْكِيْرُ خَبَثَ الْحَدِيْدِ وَالذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ وَلَيْسَ لِلْحَجَّةِ الْمَبْرُورَةِ ثَوَابٌ إِلاَّ الْجَنَّةُ))

“ Fuatanisheni baina ya Hija na Umra, kwani viwili hivyo huondoa ufakiri na madhambi kama vile kiriba cha moto kinavyoondoa uchafu katika chuma na dhahabu na fedha, na hakuma malipo ya Hija iliokubaliwa isipokuwa pepo”.

Enyi Waislamu :

Hakika Hija ina nguzo zake maalum zenye hikma nyingi na ujira mkubwa.

Anasema ALLAH (SW) :

{ ثُمَّ لْيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلْيُوفُوا نُذُورَهُمْ وَلْيَطَّوَّفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ * ذَلِكَ وَمَن يُعَظِّمْ حُرُمَاتِ اللَّهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَّهُ عِندَ رَبِّهِ }
الحج 29 - 30

“ Kisha wajisafihe taka zao, na watimize nadhiri zao, na waizunguke nyumba ya kale (Al-Kaaba). Namna hivi iwe, na anaevitukuza vitakatifu vya ALLAH basi hiyo ni kheri yake mwenyewe mbele ya Mola wake ”.

Katika aya hii imekhusishwa Baitul Haram kwani hiyo ndio nyumba pekee inayokusudiwa kwa ziara wakati wa Hija. Na tawafu humo ni katika nguzo

bora, na yameshurutishwa katika tawafu yale yalioshurutishwa katika sala miongoni mwa tohara na kujistiri.

Imepokewa kutoka kwa Ibnu Abbas (ra) yakuwa Mtume (saw) kasema :

((اَلطَّوَافُ حَوْلَ الْبَيْتِ صَلاَةٌ إِلاَّ أَنَّكُمْ تَتَكَلَّمُونَ فِيْهِ فَمَنْ تَكَلَّمَ فِيْهِ فَلاَ يَتَكَلَّمُ إِلاَّ بِخَيْرٍ))

“ Tawafu ya kuizunguka Al-Kaaba ni sala, isipokuwa nyinyi mnazungumza ndani yake, basi atakaezungumza wakati wa tawafu asizungumze isipokuwa mambo ya kheri ”.

Na sharti ya tawafu ni kuiweka Al-Kaaba upande wa kushoto wakati unatufu kama alivyofanya Mtume (saw), na haya ni kuwakhalifu washirikiana kwani wao walikuwa wanaiweka upande wa kulia wakati wanapotufu.

Ndugu Waislamu :

Anatakiwa kila mwenye kuhiji ajidhalilishe mbele ya Mola wake na awe mwenye kuomba maghfira kwa wingi, na hatakiwi kudhihirisha utukufu kwa kujipamba au kutumia manukato au kuvaa nguo za fakhari.

Imepokewa kutoka kwa Ibnu Umar (ra) yakuwa amesema :

“Alikuja mtu kwa Mtume (saw) akamuuliza” : “Ni nani mwenye kuhiji ?“ *Mtume (saw) akamjibu :*

((اَلشَّعْثُ التَّفِلُ))

“ Mwenye kuacha mapambo na manukato ”.

Enyi Waja wa ALLAH :

Katika nguzo muhimu za Hija ni kusimama Arafati , na hana hija yule alieikosa nguzo hii.

Amesema Mtume (saw) :

((اَلْحَجُّ عَرَفَةُ مَنْ جَاءَ لَيْلَةَ جَمْعٍ قَبْلَ طُلُوعِ الْفَجْرِ فَقَدْ أَدْرَكَ الْحَجَّ))

“ Hija ni Arafa, na atakaefika hapo usiku wa kuamkia tarehe 9 kabla ya alfajiri, huwa ameiwahi Hija”.

Na katika sharia kisimamo cha Arafat huanza adhuhuri siku ya tarehe 9 Mwezi wa Dhul Qaada (Mfungo 3) mpaka baada ya kutua jua siku hiyo, na hawatakiwi mahujaji kuondoka hapo kuelekea Muzdalifa ila baada ya jua kutua.

Enyi Waislamu :

Katika mambo ambayo ALLAH (SW) ameyafaridhisha kwa Nabii Ibrahimu (as) wakati wa Hija ni kutembea baina ya majabali mawili ya Safaa na

Marwa, kama walivyofanya hayo mke wake Hajara na mwanawe Ismail walipokuwa wakitafuta maji. Na walikuwa Waarabu wakati wa jahilia wakifanya hayo, ulipokuja Uislamu uliyakubali baadhi ya matendo yao ya Hija yalio mazuri na kuyakataa yale maovu.
Ilipokuja amri ya kufanya Saa'yi, Maansari walimwambia Mtume (saw) :
" Hakika sisi tulikuwa tunaona uzito kufanya Saa'yi baina ya Safaa na Marwa wakati wa jahilia.
ALLAH (SW) akateremsha aya isemayo :

{إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِن شَعَآئِرِ اللّهِ فَمَنْ حَجَّ الْبَيْتَ أَوِ اعْتَمَرَ فَلاَ جُنَاحَ عَلَيْهِ أَن يَطَّوَّفَ بِهِمَا } البقرة158

" Hakika Safaa na Marwa ni katika alama za kuadhimisha dini ya ALLAH, basi anaehiji kwenye nyumba hiyo au kufanya umra, si kosa kwake kuvizunguka vilima hivyo viwili".

فَاتَّقُوا اللهَ – عِبَادَ اللهِ – وَحَافِظُوا عَلَى شَعَائِرِ الإِسْلاَمِ وَمَعَالِمِ الإِيْمَانِ وَمَنَازِلِ الإِحْسَانِ تُدْرِكُوا جَنَّةَ الرِّضْوَانِ .

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ ، أَقُوْلُ قَولِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الْكَرِيْمُ .

*** *** ***

اَلْحَمْدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ، وَلاَ عُدْوَانَ إِلاَّ عَلَى الظَّالِمِينَ . وَنَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ وَلِيُّ الصَّالِحِينَ ، وَنَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ إِمَامُ الأَنْبِيَاءِ وَالْمُرْسَلِينَ ، وَأَفْضَلُ خَلْقِ اللهِ أَجْمَعِينَ ، صَلَوَاتُ اللهِ وَسَلاَمُهُ عَلَيْهِ ، وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَالتَّابِعِينَ لَهُمْ بِإِحْسَانٍ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عَبَادَ اللهِ :

Enyi Waislamu :
Wanatakiwa mahujaji wajipambe kwa tabia nzuri na uchamungu wanapokuwa wanatekeleza ibada hii tukufu ya Hija. Hivyo, haitakiwi kabisa kwa mwenye kuhiji kuzungumza au kufanya mambo machafu au hata kubishana na wenziwe.
Anasema ALLAH (SW) :

{ الْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَاتٌ فَمَنْ فَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ فَلاَ رَفَثَ وَلاَ فُسُوقَ وَلاَ جِدَالَ فِي الْحَجِّ } البقرة197

“Hija ni miezi maalum, na anaekusudia kufanya hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asibishane katika hija”.

Na amesema Mtume (saw) :

((مَنْ حَجَّ فَلَمْ يَرْفُثْ وَلَمْ يَفْسُقْ رَجَعَ مِنْ ذُنُوبِهِ كَيَوْمٍ وَلَدَتْهُ أُمُّهُ))

“ Atakaehiji akawa hakusema maneno machafu wala hakufanya matendo maovu hurejea hali ya kuwa hana dhambi kama siku aliozaliwa na mama yake”.

Enyi Waislamu :

Hakika Hija ni ibada ya kiwiliwili na mali, na yale yalolazimishwa katika Hija miongoni mwa sadaka na kuchinja, humtakasa mwenye kuhiji kutokana na ubakhili.

Ndio maana alipoulizwa Mtume (saw) : “Ni Hija ipi ilo bora ?” Akajibu :

((اَلْعَجُّ وَالثَّجُّ))

“ Ni ile ambayo Talbia yake imepigwa kwa sauti kubwa na iliochinjiwa mnyama ”.

Na amesema Mtume (saw) :

(اَلْحِجُّ الْمَبْرُورُ لَيْسَ لَهُ جَزَاءٌ إِلاَّ الْجَنَّةُ : قِيْلَ: وَمَا بِرُّهُ ؟ : قَالَ : إِطْعَامُ الطَّعَامِ وَطِيْبُ الْكَلاَمِ)

“ Hija iliofanywa vizuri na kubaliwa haina malipo isipokua pepo”. Wakauuliza Masahaba : Ni nini wema wake ? Akasema : “ Kulisha masikini na kusema maneno mazuri ”.

Enyi waja wa ALLAH :

Mcheni ALLAH Mola wenu Mtukufu. Fanyeni mambo ya kheri mpate kufuzu duniani na akhera. Ikimbilieni Hija wakati munaweza kuitimiza kabla hamjazuilika nayo ili mpate msamaha na radhi za Mola wenu.

فَاتَّقُوا اللهَ – يَا عِبَادَ اللهِ – وَافْعَلُوا الْخَيْرَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ، وَتَعَجَّلُوا الْحَجَّ فَإِنَّ أَحَدَكُمْ لاَ يَدْرِي مَاذَا يَعْرِضُ لهُ

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَاإِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى . اللهم أَعِزَّ الإسلامَ والمسلمين،وأَذِلَّ الشركَ والمشركين، ودَمِّرِ اللّهُمَّ جميعَ أعداءِ الحقِّ والدينِ .

"ربنا ءاتنا من لدنك رحمة وهيئ لنا من أمرنا رشدا".

اللهم استخلِفْنَا في أرضِكَ كما استخلفتَ مَنْ قَبْلَنَا من عِبَادِكَ المُؤْمِنينَ، ومَكِّنْ لَنا دِينَنَا الذي ارتَضَيتَهُ لنا، وأَبْدِلْنَا بِخَوفِنَا أَمْنَا،وبِذُلِّنَا عِزّا،وبِفَقْرِنَا غِنًى، وبِتَشَتُّتِنَا وَحْدَةً، واجْمَعْنا عِلى كلمتك،وألِّفْ بين قُلوبِنا بطاعتك.

اللهم إنَّا ضُعفاءُ فَقَوِّنَا، وإنَّا أذلاءُ فأعِزَّنَا، وإنا فقراء فَأَغْنِنَا ، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام،وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خَلِّصِ المَسجدَ الأقصى وسائرَ بِلادِ المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، وَاجْعَلْهاَ في أيدي عِبادِك المؤمنين،الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار".

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ

KUUPOKEA MWAKA MPYA WA KIISLAMU

بسم الله الرحمن الرحيم

الحمد لله الذي جعل في انقضاء الليالي والأيام وتصرُّم الشهور والأعوام عبرةً للمعتبرين، وذكرى للمدكرين،أحمده تعالى بما هو له أهل من الحمد وأثني عليه، وأستغفره من جميع الذنوب وأتوب إليه، وأومن به وأتوكل عليه، من يهده الله فلا مضل له، ومن يضلل فلا هادي له،وأشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له،من يطع الله ورسوله فقد رشد،ومن يعص الله ورسوله فقد ضل ضلالا مبينا.

وأشهد ان سيدنا ونبينا محمدا عبده ورسوله، وصفيه من خلقه وخليله، بلغ الرسالة،وأدى الأمانة، ونصح الأمة، وكشف الله به الغمة،صلى الله وسلم عليه وعلى آله وصحبه وعلى التابعين لهم بإحسان إلى يوم الدين.

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلاً سَدِيداً }الأحزاب70

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ }الحشر18

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ ، وَالْعَمَلِ بِمَا فِيْهِ رِضَاهُ ، فَاتَّقُوا اللهَ وَرَاقِبُوهُ ، وَامْتَثِلُوا أَوَامِرَهُ وَلاَ تَعْصُوهُ ، وَاذْكُرُوهُ وَلاَ تَنْسَوهُ ، وَاشْكُرُوهُ وَلاَ تَكْفُرُوهُ .

Enyi waja wa Allah:

Nakuusieni na kuiusia nafsi yangu kumcha ALLAH (SW) na kushikamana na kitabu chake و kwani hiyo ndio kamba madhubuti, na fuateni sunna ya Mjumbe wake Sayyiduna Muhammad (saw) kwani hiyo ndio njia ilionyooka, kwa hakikai anaeshikana na haya hufuzu na anaeyapuuza hukhasirika

Ndugu zangu waislamu:

Tutambue ya kuwa tupo karibuni kupokea mwaka mpya wa kiislam,basi ni juu yetu kumshukuru Allah ambaye ametuwezesha kumaliza mwaka huu kwa salama na amani,na akatuwafikisha kutekeleza ibada tofauti katika masiku matukufu ya Allah ,ama kwa hakika zama zimezunguka kwa utaratibu aliouweka na kuuridhia Allah tangu siku aliyoiumba mbingu na ardhi,amesema Allah:

﴿ إِنَّ عِدَّةَ ٱلشُّهُورِ عِندَ ٱللَّهِ ٱثْنَا عَشَرَ شَهْرًا فِى كِتَٰبِ ٱللَّهِ يَوْمَ خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ مِنْهَآ أَرْبَعَةٌ حُرُمٌ ۚ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلْقَيِّمُ ۚ فَلَا تَظْلِمُوا۟ فِيهِنَّ أَنفُسَكُمْ ۚ ﴾ التوبة:

“Hakika idadi ya miezi kwa Allah ni miezi kumi na mbili katika hukumu ya ALLAH tangu alipoumba mbingu na ardhi katika hiyo iko minne mitukufu.,hio ndio dini iliyo sawa basi msidhulumu nafsi zenu humo…”.

Ndugu waumini:

Kwa hakika tarekhe ya kiislamu imewekwa sambamba na tukio la hijra ya mtume (s.a.w),kwa kuwa hijra ndio zalio la haki,na kun’gaa kwa nuru ya imani katika ulimwengu na kuanza kwa dola ya kiislamu na kuwa imara,basi hapo uongofu wa Allah aliomtuma nao bwana wetu mtume ()ukasambaa katika mataifa ya ulimwengu amesema Allah:

”﴿ هُوَ ٱلَّذِىٓ أَرۡسَلَ رَسُولَهُۥ بِٱلۡهُدَىٰ وَدِينِ ٱلۡحَقِّ لِيُظۡهِرَهُۥ عَلَى ٱلدِّينِ كُلِّهِۦ وَلَوۡ كَرِهَ ٱلۡمُشۡرِكُونَ ٣٣ ﴾ التوبة: ٣٣”

“Yeye ndiye aliyemtuma mtume wake kwa uwongofu na dini ya haki ipate kushinda dini zote,ijapokuwa washirikina watachukia”.

ENYI Waja wa ALLAH:

Kwa ajili hio inapasa kwa umma wa kiislamu kushikamana na tarekhe ya kiislamu ambayo ALLAH ameijalia ktk miezi kumi na mbili, tarekhe ambayo imebeba matukio mbalimbali makubwa yanayohusu dini yetu,na uislamu ukaambatanisha kwa tarekhe hio hukumu mbali mbali za kisheria ambazo ni lazima zihesabiwe kwa tarekhe hio kama vile;ada za wanawake na eda zao,na funga na ibada za hija,na zaka,na hukumu mbali mbali za mirathi na mengineyo,amesema ALLAH:

”﴿ ۞ يَسۡـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلۡأَهِلَّةِۖ قُلۡ هِىَ مَوَٰقِيتُ لِلنَّاسِ وَٱلۡحَجِّۗ ﴾ البقرة: ١٨٩”

“Wanakuuliza khabari ya miezi ,sema; hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na hija..”.

نفعني الله وإياكم بهدي كتابه،أقول قولي هذا،وأستغفر الله لي ولكم فاستغفروه يغفر لكم ،وادعوه يستجب لكم إنه هو البر الكريم.

الحمد لله رب العالمين،والعاقبة للمتقين ، ولا عدوان إلا على الظالمين، وأشهد أن لا إله إلا الله ولي الصالحين، وأشهد أن سيدنا محمدا عبده ورسوله سيد الأولين والآخرين، وخاتم النبيين والمرسلين صلى الله وسلم عليه وعلى آله وصحبه ، وعلى كل من سار على نهجه إلى يوم الدين. أما بعد:

Ndugu waislamu:

Kwa hakika kukatika miezi na miaka ni jambo linalohitajia mazingatio zaidi,na kwamba kila siku inayopita ktk umri wa mwanadamu basi atambue mwanadamu huyo ya kuwa amepoteza rasili mali kubwa ktk uhai wake,kwa hakika tarekhe ni shahidi kwa mwanadmu na kila ambacho akitendacho ataiona athari ytake katika uhai wake wa baadae,imepokelewa ya kuwa Imam Al-Hasan Al- basary:

" ما من يوم يَنْشَقُّ فَجرُهُ إلا وينادي: يا ابنَ آدم أنا خَلْقٌ جديدٌ، وعلى عملك شهيد، فَتَزَوَّدْ مني فإني إذا مضيتُ لا أعود إلى يوم القيامة".

Hakuna siku yoyote ambayo inapambazuka alfajiri yake ila siku hiyo hunadi :ewe mwanadamu hakika mimi ni kiumbe mpya,na mimi ni shahidi juu ya vitendo vyako basi vuna kheri kuna kwangu kwani mimi nikiondoka sirudi tena mpaka siku ya kiama”

Ndugu waumini:

Tujihimu katika jambo la uchamungu ,na kuzihisabu nafsi zetu kwenye ukingo wa mwaka huu kwa kuchukuwa mafunzo kwa yale yalitutangulia krk mwaka huu na kujiandaa wa masiku yajao kwa uwezo wa Allah,basi ikiwa kuna kheri tumeifanya katika mwaka huu tumshukuru ALLAH kwani ni kwa tawfiqi yake na rehma yake,na ikiwa kuna maasi tuliyatenda basi kutubia kwa Allah na kujikomboa na athari ya maasi hayo kabla hatujaondoka duniani,tumuombe ALLAH atuwafikishe kufanya mema zaidi katika uhai uliobakia na atufishe ktk waja wema...

هذا،وصلوا وسلموا على إمام المرسلين،وقائد الغر المحجلين،فقد أمركم الله تعالى بالصلاة والسلام عليه ، حيث قال عز قائلا عليما: "إن الله وملائكته يصلون على النبي يأيها الذين ءامنوا صلوا عليه وسلموا تسليما".

اللهم صل وسلم على محمد وعلى آل محمد،كما صليت وسلمت على إبراهيم وعلى آل إبراهيم إنك حميد مجيد،وبارك على محمد وعلى آل محمد كما باركت على إبراهيم وعلى آل إبراهيم في العالمين إنك حميد مجيد.

اللهم أعز الإسلام والمسلمين،وأذل الشرك والمشركين،ودمر اللهم جميع أعداء الحق والدين.

"ربنا ءاتنا من لدنك رحمة وهيئ لنا من أمرنا رشدا".

اللهم استخلفنا في أرضك كما استخلفت من قبلنا من عبادك المؤمنين،ومكن لنا ديننا الذي ارتضيته لنا،وأبدلنا بخوفنا أمنا،وبذلنا عزا،وبفقرنا غنى،وبتشتتنا وحدة، واجمعنا على كلمتك،وألف بين قلوبنا بطاعتك.

اللهم إنا ضعفاء فقونا، وإنا أذلاء فأعزنا، وإنا فقراء فأغننا ، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام،وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خلص المسجد الأقصى وسائر بلاد المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، واجعلها في أيدي عبادك المؤمنين،الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار" .

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

الهجرة النّبويّة

بسم الله الرّحمن الرّحيم

الحَمدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ، الذي جعل هِجرتَنا البعد عن الآثام ، والطاعة على الدّوام ، والرحمة بالأنام على مختلف السنين والأعوام . أَحْمَدُهُ سُبْحَانَهُ بِمَا هُوَ لَهُ أَهْلٌ مِنَ الْحَمْدِ وَأُثْنِي عَلَيْهِ ، وَأَسْتَغْفِرُهُ مِنْ جَمِيعِ الذُّنُوبِ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ ، وَأُومِنُ بِهِ وَأَتَوَكَّلُ عَلَيهِ ، مَنْ يَهْدِهِ اللهُ فَلاَ مُضِلَّ لَهُ ، وَمَنْ يُضْلِلْ فَلاَ هَادِيَ لَهُ . وَأَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ، الغني الحميد ، لا يقع في ملكه إلاّ ما يريد.وَأَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، سيد الشّاكرين وإمام الصّابرين . صَلَّى اللهُ عَلَيهِ وَسَلَّمَ وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ ، وَعَلَى كُلِّ مَنِ اهْتَدَى بِهَدْيِهِ وَاسْتَنَّ بِسُنَّتِهِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلاً سَدِيداً }الأحزاب70

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ }الحشر18

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ ، وَالْعَمَلِ بِمَا فِيْهِ رِضَاهُ ، فَاتَّقُوا اللهَ وَرَاقِبُوهُ ، وَامْتَثِلُوا أَوَامِرَهُ وَلاَ تَعْصُوهُ ، وَاذْكُرُوهُ وَلاَ تَنْسَوهُ ، وَاشْكُرُوهُ وَلاَ تَكْفُرُوهُ .

Ammabaad :EnyiWajawa ALLAH :

Hakika Hijra ya Mtume (saw) ina mafunzo na mazingatio yasio malizika katika nyoyo za Waislamu. Na katika hayo ni kwa Muislamu kuhama kutoka katika mji wake na kwenda katika mji mwengine kwa lengo la kuyakimbia maasi na kutafuta radhi za Mola wake. Kama alivyofanya hayo Mtume (saw) pale alipohama Makka na akahamia Madina.

Amesema Mtume (saw) :

((اَلْمُهَاجِرُ مَنْ هَجَرَ مَا نَهَى اللهُ عَنْهُ))

" Mwenye kufanya hijra ni Yule anaeyakimbia yale yaliokatazwa na ALLAH ".

وقال أيضا : ((اَلْمُهَاجِرُ مَنْ هَجَرَ الْخَطَايَا وَالذُّنُوبَ))

“ Mwenye kufanya hijra ni Yule anae yakimbia makosa na madhambi ”.

وقال أيضا : ((اَلْمُهَاجِرُ مَنْ هَجَرَ السُّوءَ فَاجْتَنَبَهُ))

“ Mwenye kufanya hijra ni Yule anaeyakimbia maovu na akajitenga nayo”.

Mafunzo haya yanamuhusu kila Muislamu wakati wowote na pahala popote alipo, kwani matokeo yote ya kiislamu hayawi kwa watu maalum wala kwa wakati maalum, bali ni ya Waislamu wote hata kama hawaja yashuhudia yalipotokea.

Anasema ALLAH (SW) :

{ لَقَدْ كَانَ فِي قَصَصِهِمْ عِبْرَةٌ لِّأُوْلِي الأَلْبَابِ مَا كَانَ حَدِيثاً يُفْتَرَى وَلَكِنْ تَصْدِيقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ كُلَّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ } يوسف 111

“ Bila ya shaka katika hadithi zao hizi limo fundisho kwa wenye akili, sio maneno yaliozuliwa bali ni hakikisho la yale yalio kuwa kabla yake, na pia ni maelezo ya kila kitu, na ni uongofu na rehma kwa watu wenye kuamini ”.

Hijra pia inatufunza kuwa tuwe na ikhlas katika matendo yetu, na yote tunayoyafanya yawe ni kwa kutaka radhi za Mola wetu, na daima tumtegemee ALLAH (SW) katika mambo yetu yote, tuwe wakweli katika nafsi zetu na tuwe tunapendana na kusaidiana katika shida na raha, na hivi ndivyo walivyokuwa watangulizi wetu wema.

Amesema Mtume (saw) :

((إِنَّمَا الأَعْمَالُ بِالنِّيَاتِ وَإِنَّمَا لِكُلِّ امرِئٍ مَا نَوَى فَمَنْ كَانَتْ هِجْرَتُهُ إِلَى اللهِ وَرَسُولِهِ فَهِجْرَتُهُ إِلَى اللهِ وَرَسُولِهِ وَمَنْ كَانَتْ هِجْرَتُهُ إِلَى دُنْيَا يُصِيبُهَا أَوْ إِلَى امْرَأَةٍ يُنْكِحُهَا فَهِجْرَتُهُ إِلَى مَا هَاجَرَ إِلَيْهِ))

“ Hakika amali hulipwa kwa nia zake, na kila mtu hulipwa kwa nia yake, yule ambae hijra yake ni kwa ajiliya ALLAH na Mtume wake basi hijra yake itakua ni kwa ajili ya ALLAH naMtume wake, na Yule ambae hijra yake ni kwa ajili ya kupata dunia au mwananamke amuoe, basi hijra yake itakuwa kwa yale alioyafatia ”.

Na amesimulia Ibnu Masoud (ra) kuwa :

“ Miongoni mwetu alikuwepo mtu aliemposa mwanamke anaeitwa Ummu Qais, Yule bibi akakataa kuolewa mpaka kwanza huyu bwana ahame, basi Yule mtu akahama na akamuoa Yule mwanamke, nasi tukawa tunamwita mtu huyu; aliehama kwa ajili ya Ummu Qais”.

PiaHijra inatufunza kuwa wakarimu kwa wageni wetu na wala tusiwe mabakhili, kama ilivyotokea wakati Mtume (saw) alipojiwa na mgeni na akawa hana cha kumkirimu, akawataka Masahaba wake wamchukue na wamkirimu siku ile, na Masahaba wakafanya hayo haliyakuwa wao wenyewe hawana kitu.

ALLAH (SW) akateremsha aya isemayo :

{ وَيُؤْثِرُونَ عَلَى أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ } الحشر 9

“ Na wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wao wenyewe ni wahitaji ”.

Na ALLAH (SW) anasema :

{ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُوْلَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ } الحشر 9

“ Na waepushwao na ubakhili wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kweli kweli”.

EnyiWajawaALLAH :
HakikaUislamu unatuamrisha kuisimamia ipasavyo dini yetu na pia kuimarisha dunia yetu, kwani Hijra inatufunza kuwa, baada ya mtu kuhama na kwenda katika mji mwengine basi atafute rizki yake huko kwa kufanya kazi za halali na wala asikae huku akitegemea misaada kutoka kwa wenyeji wake, kama alivyofanya hayo Abdulrahman bin Auf (ra) kwa kufanya biashara katika soko la Madina baada ya kuhamia huko. Saad bin Al-Rabii Al-Ansary alitaka kumgaia Abdulrahman bin Auf (ra) nusu ya mali yake lakini alikataa na akajitegemea mwenyewe kwa kufanya biashara.

Anasema ALLAH (SW) :

{ وَلاَ تَنسَ نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا وَأَحْسِن كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ وَلاَ تَبْغِ الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ إِنَّ اللَّهَ لاَ يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ } القصص 77

“ Na wala usisahau sehemu yako ya dunia na ufanye wema kama ALLAH alivyokufanyia, wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi, bilaya shaka ALLAH hawapendi mafisadi ”.

Na anasema ALLAH (SW) :

{ وَقُلِ اعْمَلُواْ فَسَيَرَى اللّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ وَسَتُرَدُّونَ إِلَى عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ } التوبة 105

" Nasema : Tendeni mambo mazuri, ALLAH atayaona mambo yenu hayo na Mtume wake na Waislamu. Na mtarudishwa kwa Mjuzi wasiri na dhahiri, nae atakwambieni yote mlio kuwa mkiyatenda ".

فَاتَّقُوا اللهَ – عِبَادَ اللهِ – واستلهموا من هجرة النبي الكريم الدروس والعبر ، واجعلوا أيامكم مملوءة بالطاعة وهي من معاني الهجرة العظيمة .

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ ، أَقُوْلُ قَولِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الْكَرِيْمُ .

*** *** ***

اَلْحَمْدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ، وَلاَ عُدْوَانَ إِلاَّ عَلَى الظَّالِمِينَ . وَنَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ وَلِيُّ الصَّالِحِينَ ، وَنَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ إِمَامُ الأَنْبِيَاءِ وَالْمُرْسَلِينَ ، وَأَفْضَلُ خَلْقِ اللهِ أَجْمَعِينَ ، صَلَوَاتُ اللهِ وَسَلاَمُهُ عَلَيْهِ ، وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَالتَّابِعِينَ لَهُمْ بِإِحْسَانٍ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ :

Enyi Waja waALLAH :

Hakika kuanza kwa tarehe ya Kiislamu kumenasibishwa natukio la Hijra ambalo lilifanyika katika mwezi wa Muharram, na Masahaba waliinasibisha tarehe ya Kiislamu na tukio la Hijra kwa kufuata kauli ya ALLAH (SW) isemayo :

{ لَمَسْجِدٌ أُسِّسَ عَلَى التَّقْوَى مِنْ أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَن تَقُومَ فِيهِ } التوبة 108

“ Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa uchamungu tangu siku ya kwanza (ya kufika Mtume (saw) Madina) unastahiki zaidi wewe usimame humo ”.

Ni dhahiri kwamba hapa haijakusudiwa siku ya mwanzo aliohamia Mtume (saw) Madina, lakini umekusudiwa wakati yalipoanza kudhihiri mafunzo na utamaduni wa Kiislamu baada ya Mtume (saw) na Masahaba wake kufika Madina na kujenga msikit wa mwanzo katika Uislamu. Msikiti huu unaitwa Masjid Qubaa. Na hii ni dalili tosha ya umuhimu wa msikiti katika jamii ya waislamu.

Enyi Waja wa ALLAH :

Mcheni ALLAH Mola wenu Mtukufu, utumieni ukumbusho huu kwa kuyakimbia maasi na kujikaribisha kwake kwa kufanya mambo ya kheri ya takayoupeleka mbele Uislamu, kama kujenga misikiti, madaris, kusomesha elimu na mambo mengineyo.

Upokeeni mwaka huu mpya wa kiislamu kwa furaha, jiandaeni kuutumia wakati wake vizuri, na tufikirini sana jinsi tulivyoutumia mwaka uliopita.

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَاإِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى . اللهم أَعِزَّ الإسلامَ والمسلمين،وأَذِلَّ الشركَ والمشركين، ودَمِّرِ الّلهُمَّ جميعَ أعداءِ الحقِّ والدينِ .

"ربنا ءاتنا من لدنك رحمة وهيئ لنا من أمرنا رشدا".

اللهم استخلِفْنَا في أرضِكَ كما استخلفتَ مَنْ قَبْلَنَا من عِبَادَك المُؤْمِنينَ، ومَكِّنْ لَنا دِينَنَا الذي ارتَضَيتَهُ لنا، وأَبْدِلْنَا بِخَوفِنَا أَمْنَا،وبِذُلِّنَا عِزّا،وبِفَقْرِنَا غِنًى، وبِتَشَتُّتِنَا وَحْدَةً، واجْمَعْنا عِلى كلمتك،وألِّفْ بين قُلوبِنا بطاعتك.

اللهم إنَّا ضُعفاءُ فَقَوِّنَا، وإنَّا أذلاءُ فأعِزَنَا، وإنا فقراء فَأَغْنِنَا ، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام،وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خَلِّصِ المَسجدَ الأقصى وسائرَ بِلادِ المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، وَاجْعَلْهاَ في أيدي عِبادِك المؤمنين،الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار".

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

شوال الآداب الشّرعيّة في السّوق .

بسم الله الرّحمن الرّحيم

الحَمدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ، أَحْمَدُهُ سُبْحَانَهُ بِمَا هُوَ لَهُ أَهْلٌ مِنَ الْحَمْدِ وَأُثْنِي عَلَيْهِ ، وَأَسْتَغْفِرُهُ مِنْ جَمِيعِ الذُّنُوبِ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ ، وَأُومِنُ بِهِ وَأَتَوَكَّلُ عَلَيهِ ، مَنْ يَهْدِهِ اللهُ فَلاَ مُضِلَّ لَهُ ، وَمَنْ يُضْلِلْ فَلاَ هَادِيَ لَهُ . وَأَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ يُحْيِ وَيُمِيتُ وَهُوَ حَيٌّ لاَ يَمُوتُ بِيَدِهِ الْخَيْرُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ . وَأَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ ، سَيِّدُ خَلْقِهِ وَخَاتِمُ أَنْبِيَائِهِ ، صَلَّى اللهُ عَلَيهِ وَسَلَّمَ وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ ، وَعَلَى كُلِّ مَنِ اهْتَدَى بِهَدْيِهِ وَاسْتَنَّ بِسُنَّتِهِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلاً سَدِيداً }الأحزاب70

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ }الحشر18

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ ، وَالْعَمَلِ بِمَا فِيْهِ رِضَاهُ ، فَاتَّقُوا اللهَ وَرَاقِبُوهُ ، وَامْتَثِلُوا أَوَامِرَهُ وَلاَ تَعْصُوهُ ، وَاذْكُرُوهُ وَلاَ تَنْسَوهُ ، وَاشْكُرُوهُ وَلاَ تَكْفُرُوهُ .

Enyi Waja wa ALLAH :

Mcheni ALLAH kama ipasavyo kumcha, fuateni maamrisho yake wala msimuasi, mdhukuruni wala msimsahau, na mshukuruni wala msimkufuru.

Na tambueni kuwa Uislamu umeweka adabu na taratibu nyingi ambazo tunatakiwa tuzifuate tunapokwenda sokoni. Na sisi katika haya, tunatakiwa tumfuate Mtume (saw) kwani yeye alikuwa haoni uovu ila huukataza na kuondoa na haoni wema ila huukubali na kuuhimiza.

Katika adabu za sokoni ni kuwa imesunniwa anaeingia sokoni kwanza amdhukuru ALLAH (SW) na kumsifu. Kwani imepokewa kutoka Sayyiduna Umar (ra) ya kuwa Mtume (saw) amesema :
“ Atakaeingia sokoni akasema :

((لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ ، يُحْيِى وَيُمِيْتُ وَهُوَ حَيٌّ لاَ يَمُوْتُ ، بِيَدِهِ الْخَيْرُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ)) .

ALLAH humuandikia mema mengi sana, humfutia maovu mengi sana, humpandisha daraja nyingi sana na humjengea nyumba katika pepo ".

Na haipendezi kwa anaeingia sokoni kujadiliana au kupatana sana kwa sauti kubwa, kwani imepokewa kutoka kwa Abdulla bin Umar (ra) kwamba, miongoni mwa tabia na sifa za Mtume (saw) ni kuwa :
Hakuwa mtu mkali mwenye moyo mgumu, wala hakuwa mwenye kujadiliana sokoni, wala hakuwa akilipa uovu kwa uovu, bali alikuwa ni mwenye kusamehe.

Enyi waja Wa ALLAH :
Na katika adabu za sokoni ni kutoa salamu wakati wa kuingia, kwa vile sokoni kuna watu wengi watakaoitikia salamu hiyo na kumzidishia ujira yule alieitoa.
Amesema Mtume (saw) :

((لاَ تَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ حَتَّى تُؤْمِنُوا ، وَلاَ تُؤْمِنُونَ حَتَّى تَحَابُّوا ، أَوَلاَ أَدُلُّكُمْ عَلَى شَيْءٍ إِذَا فَعَلْتُمُوهُ تَحَابَبْتُمْ ، أَفْشُوا السَّلاَمَ بَيْنَكُمْ))

" Hamtoingia peponi mpaka muamini, na wala hamtoamini mpaka mpendane, jee nisikujuulisheni kitu ambacho mkikifanya mtapendana, toleaneni salamu baina yenu ".

Na katika adabu za sokoni ni kufanya mambo kwa wepesi na masikilizano wakati wa kuuza na kununua.
Amesema Mtume (saw) :

((رَحِمَ اللهُ عَبْدًا سَمْحًا إِذَا بَاعَ ، سَمْحًا إِذَا اشْتَرَى ، سَمْحًا إِذَا اقْتَضَى))

" ALLAH anamrehemu mja alie msamehevu anapouza, alie msamehevu anaponunua na alie msamehevu anapodai ".

Enyi Waja wa ALLAH :
Anatakiwa Muislamu anapofanya biashara zake ajiepushe na kula viapo vya uongo, kwani viapo hivyo ingawa vinasaidia katika kuuza lakini vinaondoa baraka katika biashara.
Amesema Mtume (saw) :

((اَلْحَلِفُ مَنْفَقَةٌ لِلسِّلْعَةِ ، مَمْحَقَةٌ لِلْبَرَكَةِ))

" Kiapo kinasaidia kwenye kuuza, lakini kinaondoa baraka ".

Na amesema vile vile :

((إِيَّاكُمْ وَكَثْرَةِ الْحَلْفِ فِيْ الْبَيْعِ ، فَإِنَّهُ يُنْفِقُ ثُمَّ يُمْحِقُ))

“ Tahadharini na viapo vingi katika kuuza, kwani viapo husaidia kuuza kisha huondoa baraka ”.

Na ni juu ya Muislamu vile vile kujiepusha na khadaa ya aina yoyote au kughushi katika biashara zake.
Amesema Mtume (saw) baada ya kumuona mtu anafanya khadaa sokoni :

((مَنْ غَشَّنَا فَلَيْسَ مِنَّا))

“ Anaetufanyia ghushi (hadaa) hayupo katika sisi ”.

Na amesema Mtume (saw) :

((اَلْخَدِيْعَةُ فِيْ النَّارِ))

“ Khadaa hupelekea motoni ”.

Na ni juu ya Muislamu vile vile kujiepusha na wizi wa kupunguza vipimo anapopima kwa mizani au kipimo chochote anachokitumia.
Anasema ALLAH (SW) :

(وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيْمِ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيْلاً) الإسراء35

“ Na timizeni kipimo mpimapo, na pimeni kwa mizani zilizo sawa, hayo ni wema kwenu na bora mwishoni (kwake) ”.

Na anasema ALLAH (SW) katika kutueleza malipo wa wapunjaji :

(وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِيْنَ * اَلَّذِيْنَ إِذَا اكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُوْنَ * وَإِذَا كَالُوْهُمْ أَوْ وَّزَنُوهُمْ يُخْسِرُوْنَ) المطففين 1–3

“ Maangamizo yatawathubutukia wapunjao. Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea kipimo kamili. Lakini wanapowapimia watu kwa kibaba au mizani wao hupumguza ”.

Bila ya shaka, wafanyao haya wamesahau kufufuliwa na wameisahau siku ya malipo.
ALLAH (SW) anawauliza :

(أَلاَ يَظُنُّ أُولَئِكَ أَنَّهُمْ مَّبْعُثُونَ * لِيَوْمٍ عَظِيْمٍ * يَوْمَ يَقُوْمُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعَالَمِيْنَ) المطففين4–6

“ Jee, wao hawafikiri kuwa watafufuliwa? Katika siku ilio kuu.
Siku watakaposimama watu mbele ya Mola wa walimwengu wote ”.

Na katika yanayokatazwa kwa wafanya biashara ni kuficha bidhaa muhimu ili zipate kuadimika na hatimae kupanda bei.
Amesema Mtume (saw) :

((لاَ يَحْتَكِرُ إِلاَّ خَاطِئٌ))

“ Hafichi bidhaa isipokuwa mtu mwenye kufanya makosa ”.

Na amesema Mtume (saw) :

((مَنِ احْتَكَرَ عَلَى الْمُسْلِمِيْنَ طَعَامًا ضَرَبَهُ اللهُ بِالْجُذَامِ وَالإِفْلاَسِ))

“ Atakaewafichia Waislamu chakula, ALLAH atamuadhibu kwa maradhi ya ukoma na kufilisika ”.

فَاتَّقُوا اللهَ – عِبَادَ اللهِ – وَامْتَثِلُوا سُنَنَ الْهُدَى فِي أَسْوَاقِكُمْ تُفْلِحُوا ، وَاجْتَنِبُوا فِيْهَا مَسَالِكَ الرَّدَى تَرْبَحُوا .

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ ، أَقُوْلُ قَولِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الْكَرِيْمُ .

*** *** ***

اَلْحَمْدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ، وَلاَ عُدْوَانَ إِلاَّ عَلَى الظَّالِمِينَ . وَنَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ وَلِيُّ الصَّالِحِينَ ، وَنَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ إِمَامُ الأَنْبِيَاءِ وَالْمُرْسَلِينَ ، وَأَفْضَلُ خَلْقِ اللهِ أَجْمَعِينَ ، صَلَوَاتُ اللهِ وَسَلاَمُهُ عَلَيْهِ ، وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَالتَّابِعِينَ لَهُمْ بِإِحْسَانٍ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عَبَادَ اللهِ :

Enyi Waja wa ALLAH :
Katika mambo muhimu yanayomuwajibikia mfanya biashara ni kuwa na elimu ya dini juu ya mambo ya biashara ili aweze kupambanua baina ya pato la halali na pato la haramu katika kazi zake.
Mtume (saw) ametuonya juu ya hayo aliposema :

((يَأْتِى عَلَى النَّاسِ زَمَانٌ لاَ يُبَالِي الْمَرْءُ مَا أَخَذَ مِنْهُ أَمِنَ الْحَلاَلِ أَمْ مِنَ الْحَرَامِ))

" Zitakuja zama kwa watu itakuwa mtu hajali juu ya anachokichukua, jee ni katika halali au katika haramu ".

Na imepokewa kuwa Sayyiduna Umar ibnu Al-Khattab (ra) amesema :

((لاَ يَبِعْ فِيْ سُوْقِنَا إِلاَّ مَنْ قَدْ تَفَقَّهَ فِيْ الدِّيْنِ))

" Asifanye biashara katika soko letu ila yule mwenye elimu ya dini ".

Pia inasimuliwa kuwa, mmoja wa watangulizi wetu wema (Salafu Salih) alikuwa na mtoto alietaka kufanya biashara. Mzazi huyu alimuuliza mwanawe masuala mengi ya dini yanayokhusu biashara, na yule mtoto aliyajibu masuala yote hayo kwa usahihi isipokuwa alishindwa kulijibu suala moja tu. Yule mzee akamwambia mwanawe :

((اِجْلِسْ يَا بُنَيَّ لاَ تُطْعِمْنَا الْحَرَامَ))

" Kaa Ewe mwanangu (usifanye biashara) usitulishe haramu ".

Enyi Waja wa ALLAH :
Mcheni ALLAH Mola wenu alietukuka, jifunzeni misingi ya dini yenu kwa ukamilifu, na fanyeni biashara zenu kwa kufuata misingi ya sharia za dini yenu ili pato lenu liwe la halali. Jiepusheni sana na kila chumo la haramu, kwani pato la haramu halipelekei isipokuwa motoni.
Amesema Mtume (saw) :

((إِنَّ التُّجَّارَ يُبْعَثُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فُجَّارًا إِلاَّ مَنِ اتَّقَى اللهَ وَبَرَّ وَصَدَقَ))

" Hakika wafanya biashara watafufuliwa siku ya Qiyama hali ya kuwa ni waovu, isipokuwa yule mwenye kumuogopa ALLAH na akafanya wema na akasema kweli katika biashara yake ".

Na pia amesema Mtume (saw) :

((إِنَّ التُّجَّارَ هُمُ الْفُجَّارُ . قَالُوا : يَا رَسُولَ اللهِ أَلَيْسَ قَدْ أَحَلَّ اللهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا ؟ قَالَ : بَلَى وَلَكِنَّهُمْ يَحْلِفُونَ وَيَأْثَمُوْنَ))

" Hakika wafanya biashara wao ni waovu. Wakasema Masahaba : Ewe Mjumbe wa ALLAH, kwani ALLAH (SW) hakuhalalisha biashara na hakuharamisha riba ? Akasema Mtume (saw) : Ni sawa lakini wao (wafanya biashara) wanaapa (viapo vya uongo) na wanafanya uovu ".

فَاتَّقُوا اللهَ – عِبَادَ اللهِ – وَتَفَقَّهُوا فِي أَمْرِ دِيْنِكُمْ ، وَأَقِيمُوا أَسْوَاقَكُمْ وَفْقَ شَرِيْعَةِ رَبِّكُمْ .

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ أَنْ تَرْزُقَ كُلاًّ مِنَّا لِسَانًا صَادِقًا ذَاكِرًا ، وَقَلْبًا خَاشِعًا مُنِيبًا ، وَعَمَلاً صَالِحًا زَاكِيًا ، وَعِلْمًا نَافِعًا رَافِعًا ، وَإِيمَانًا رَاسِخًا ثَابِتًا ، وَيَقِينًا صَادِقًا خَالِصًا ، وَرِزْقًا حَلاَلاً طَيِّبًا وَاسِعًا ، يَا ذَا الْجَلاَلِ وَالإِكْرَامِ.

اَللَّهُمَّ أَعِزَّ الإِسْلاَمَ وَالْمُسْلِمِينَ ، وَوَحِّدِ اللَّهُمَّ صُفُوفَهُمْ ، وَاجْمَعْ كَلِمَتَهُمْ عَلَى الْحَقِّ ، وَاكْسِرْ شَوْكَةَ الظَّالِمِينَ ، وَاكْتُبِ السَّلاَمَ وَالأَمْنَ لِعِبَادِكَ أَجْمَعِينَ .

اَللَّهُمَّ رَبَّنَا اسْقِنَا مِنْ فَيْضِكَ الْمِدْرَارِ ، وَاجْعَلْنَا مِنْ الذَّاكِرِينَ لَكَ فِي اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ، الْمُسْتَغْفِرِينَ لَكَ بِالْعَشِيِّ وَالأَسْحَارِ.

اَللَّهُمَّ أَنْزِلْ عَلَيْنَا مِنْ بَرَكَاتِ السَّمَاءِ ، وَأَخْرِجْ لَنَا مِنْ خَيْرَاتِ الأَرْضِ ، وَبَارِكْ لَنَا فِي ثِمَارِنَا وَزُرُوعِنَا يَا ذَا الْجَلاَلِ وَالإِكْرَامِ .

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ.

رَبَّنَا لاَ تُزِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ رَحْمَةً إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ .

رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنْفُسَنَا وَإِنْ لَمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِيْنَ .

اَللَّهُمَّ اغْفِرْ لِلْمُؤْمِنِينِ وَالْمُؤْمِنَاتِ ، وَالْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ ، الأَحْيَاءِ مِنْهُمْ وِالأَمْوَاتِ ، إِنَّكَ سَمِيْعٌ قَرِيْبٌ مُجِيْبُ الدُّعَاءِ .

عِبَادَ اللهِ :

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

شوال ذكر الله سلاح المؤمن .

بسم الله الرّحمن الرّحيم

الحَمدُ للهِ أَهْلِ الْحَمْدِ وَالثَّنَاءِ، وَالْمَجْدِ وَالْعِزَّةِ وَالْكِبْرِيَاءِ ، هُوَ الأَوَّلُ بِلاَ ابْتِدَاءِ ، وَالآخِرُ بِلاَ انْتِهَاءِ أَحْمَدُهُ سُبْحَانَهُ بِمَا هُوَ لَهُ أَهْلٌ مِنَ الْحَمْدِ وَأُثْنِي عَلَيْهِ ، وَأَسْتَغْفِرُهُ مِنْ جَمِيعِ الذُّنُوبِ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ ، وَأُومِنُ بِهِ وَأَتَوَكَّلُ عَلَيهِ ، مَنْ يَهْدِهِ اللهُ فَلاَ مُضِلَّ لَهُ ، وَمَنْ يُضْلِلْ فَلاَ هَادِيَلَهُ . وَأَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ، وَلاَ ضِدَّ وَلاَ شَبِيْهَ وَلاَ قَرِيْنَ مَعَهُ.وَأَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ،أَكْثَرُ الْعِبَادِ لَهْجًا بِذِكْرِ اللهِ ، وَأَطْوَعَهُمْ فِي الإِنْقِيَادِ لأَوَامِرِهِ،صَلَّى اللهُ عَلَيهِ وَسَلَّمَ وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ ، وَعَلَى كُلِّ مَنِ اهْتَدَى بِهَدْيِهِ وَاسْتَنَّ بِسُنَّتِهِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلاً سَدِيداً }الأحزاب70

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ }الحشر18

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ ، وَالْعَمَلِ بِمَا فِيْهِ رِضَاهُ ، فَاتَّقُوا اللهَ وَرَاقِبُوهُ ، وَامْتَثِلُوا أَوَامِرَهُ وَلاَ تَعْصُوهُ ، وَاذْكُرُوهُ وَلاَ تَنْسَوهُ ، وَاشْكُرُوهُ وَلاَ تَكْفُرُوهُ .

Enyi Waja wa ALLAH :

Mcheni ALLAH (SW) wala msimuasi, mdhukuruni katika nyoyo zenu, mtajeni katika midomo yenu, muombeni katika shida zenu, na mkumbukeni wala msimsahau.

Anasema ALLAH (SW) :

{وَلاَ تَكُونُوا كَالَّذِيْنَ نَسُوا اللهَ فَأَنْسَاهُمْ أَنْفُسَهُمْ أُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ}سورة الحشر 19

“ Na wala msiwe kama wale waliomsahau ALLAH, na (ALLAH) akawasahaulisha nafsi zao, hao ndio waasi wakubwa ”.

Na tambueni kuwa, kumkumbuka na kumtaja ALLAH (SW) kwa wingi ni zawadi bora ya kuichukuwa mja katika safari yake ya akhera, kwani kutokana na dhikri tunajikinga na majanga ya dunia na tunayawepesisha yaliokuwa mazito, na ndio

pepo wanayoikimbilia waja wema ambayo humrudishia mtu furaha pale anapopata huzuni na hufunganisha baina ya mja na Mola wake.

Anasema ALLAH (SW) :

{فَاذْكُرُونِي أَذْكُرْكُمْ وَاشْكُرُوا لِيْ وَلاَ تَكْفُرُونِ}سورة البقرة 152

" Na nikumbukeni nami nitakukumbukeni na mnishukuru wala msinikufuru ".

Hakika Muislamu anatakiwa amkumbuke ALLAH katika kila hali na kila wakati.
Anasema ALLAH (SW) :

{إِنَّ فِيْ خَلْقِ السَّماَوَاتِ وَالأَرْضِ وَاخْتِلاَفِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لآيَاتٍ لأُولِى الأَلْبَابِ الَّذِيْنَ يَذْكُرُونَ اللهَ قِيَامًا وَقُعُودًا وَعَلَى جُنُوبِهِمْ }سورة آل عمران 190 –191

" Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kutofautiana kwa usiku na mchana ziko hoja (za kuwepo ALLAH) kwa wenye akili, ambao humkumbuka ALLAH wakiwa wima na wakikaa na wakilala ".

Na hapana shaka kuwa, nyoyo zilizoharibika hutengenea kwa dhikri ya ALLAH kama zinavyotulia nyoyo za Waumini kwa kumkumbuka ALLAH.
Anasema ALLAH (SW) :

{الَّذِيْنَ آمَنُوا وَتَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُمْ بِذِكْرِ اللهِ أَلاَ بِذِكْرِ اللهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ } سورة الرعد 28

" Ni wale walioamini na zikatulia nyoyo zao kwa kumkumbuka ALLAH.

Sikilizeni !kwa kumkumbuka ALLAH nyoyo hutulia ".

Na imepokewa kutoka kwa Ibnu Masoud (ra), kuwa Mtume (saw) amesema :

((لَقِيْتُ إِبْرَاهِيْمَ – عَلَيْهِ السَّلاَمُ – لَيْلَةَ أُسْرِيَ بِي فَقَالَ يَا مُحَمَّدُ : أَقْرِىءْ أُمَّتَكَ مِنِّ السَّلاَمُ وَأَخْبِرْهُمْ أَنَّ الْجَنَّةَ طَيِّبَةُ التُّرْبَةِ عَذْبَةُ الْمَاءِ وَأَنَّهَا قِيْعَانٌ وَأَنَّ غِرَاسَهَا : سُبْحَانَ اللهِ وَالْحَمْدُ للهِ وَلاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَاللهُ أَكْبَرُ))

" Nilikutana na Ibrahiim (as) katika usiku wa Miiraj akasema : Ewe Muhammad ufikishie umma wako salamu zangu na waambie kuwa, pepo ina udongo mzuri na maji matamu na ni ardhi ilokaa sawa na mbegu yake ni kusema :

" سُبْحَانَ اللهِ وَالْحَمْدُ للهِ وَلاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَاللهُ أَكْبَرُ "

Enyi Waja wa ALLAH :
Mtume (saw) ametueleza fadhila za dhikri kwa kutuambia kuwa ALLAH (SW) amesema katika Hadithul Qudsiy :

((أَنَا عِنْدَ حُسْنِ ظَنِّ عَبْدِي بِي وَأَنَا مَعَهُ إِذَا ذَكَرَنِي ، فَإِنْ ذَكَرَنِي فِيْ نَفْسِهِ ذَكَرْتُهُ فِيْ نَفْسِيْ وَإِنْ ذَكَرَنِي فِيْ مَلأ ذَكَرْتُهُ فِي مَلأ خَيْرٍ مِنْهُمْ))

" Mimi niko kama vile mja wangu anavyonifikiria, na niko pamoja nae anaponitaja, akinitaja katika nafsi yake namtaja katika nafsi yangu, na akinitaja kwa watu namtaja kwa watu bora kuliko hao ".

Na amesema ALLAH (SW) katika Hadithul Qudsiy :

((مَنْ شَغَلَهُ ذِكْرِي عَنْ مَسْأَلَتِي أَعْطَيْتُهُ أَفْضَلَ مَا أُعْطِي السَّائِلِيْنَ))

" Yule ambae atashughulishwa na kunitaja mimi kuliko kuniomba, basi nitampa kilicho bora zaidi kuliko ninachowapa wale wanaoniomba ".

ALLAH (SW) anatuamrisha tudumishe dhikri yake kwa kusema :

{ فَسَبِّحْ بِحَمْد رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوْعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ الْغُرُوبِ } ق 39

" Na mtukuze Mola wako kwa kumsifu kabla ya kutoka jua na kabla ya kutua ".

Na pia anasema :

{وَاذْكُرْ رَبَّكَ فِيْ نَفْسِكَ تَضَرُّعًا وَخِيْفَةً وَدُوْنَ الْجَهْرِ مِنَ الْقَوْلِ بِالْغُدُوِّ وَالآصَالِ وَلاَ تَكُنْ مِنَ الْغَافِلِيْنَ}الأعراف 205

" Na mtaje Mola wako moyoni mwako kwa unyenyekevu na khofu bila ya kupiga kelele katika kauli (wakati wa) asubuhi na jioni, wala usiwe miongoni mwa walioghafilika ".

Na aya hii inatufahamisha kuwa, dhikri na dua zifanywe kwa sauti ndogo na wala sio kwa kupiga makelele.

Masahaba walimuuliza Mtume (saw) :
" Jee Mola wetu yupo karibu na sisi ili tumuombe kwa sauti ndogo au yuko mbali tumuombe kwa sauti kubwa".
ALLAH (SW) akateremsha aya isemayo :

{وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِيْ عَنِّيْ فَإِنِّيْ قَرِيْبٌ أُجِيْبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ}البقرة 186

" Na wakikuuliza waja wangu kuhusu mimi, waambie mimi niko karibu nao, naitikia maombi ya muombaji anaponiomba ".

Na inasimuliwa kuwa baadhi ya watu waliomba dua kwa sauti kubwa walipokuwa safarini, Mtume (saw) akawaambia :

((يَا أَيُّهَا النَّاسُ ارْبَعُوا عَلَي أَنْفُسِكُمْ فَإِنَّكُمْ لاَ تَدْعُونَ أَصَمَّ وَلاَ غَائِبًا إِنَّ الّذِيْ تَدْعُونَهُ سَمِيْعٌ قَرِيْبٌ ، أَقْرَبُ مِنْ أَحَدِكُمْ مِنْ عُنُقِ رَاحِلَتِهِ))

“ Enyi watu ! Zipunguzeni sauti zenu kwani hakika nyinyi hamumuombi kiziwi wala alie mbali, hakika huyo mnaemuomba ni mwenye kusikia na yuko karibu, yuko karibu zaidi kuliko alivyo mmoja wenu na shingo ya mnyama wake”.

فَاتَّقُوا اللهَ– عِبَادَ اللهِ– وَإِيَّاكُمْ وَالإِجْتِمَاعَ لِمَا يُسْخِطُ اللهَ سُبْحَانَهُ ، وَاحْذَرُوا مَجَالِسَ أَهْلِ الْغَفْلَةِ ، مَجَالَسَ اللَّهْوِ وَاللَّعْبِ .

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ ، أَقُوْلُ قَولِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الْكَرِيْمُ .

*** *** ***

اَلْحَمْدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ، وَلاَ عُدْوَانَ إِلاَّ عَلَى الظَّالِمِينَ . وَنَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ وَلِيُّ الصَّالِحِينَ ، وَنَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ إِمَامُ الأَنْبِيَاءِ وَالْمُرْسَلِينَ ، وَأَفْضَلُ خَلْقِ اللهِ أَجْمَعِينَ ، صَلَوَاتُ اللهِ وَسَلاَمُهُ عَلَيْهِ ، وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَالتَّابِعِينَ لَهُمْ بِإِحْسَانٍ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عَبَادَ اللهِ :

Enyi Waislamu :
Hakika watu wengi siku hizi wameghafilika na kumdhukuru ALLAH (SW) na wanatumia muda wao mwingi katika mambo ya kidunia na wanaisahau akhera, wanazungumza mambo ambayo hayawafai hapa duniani wala hayatowafaa akhera, na kufanya hivi ni kuipunguza haki ya Muumbaji na kuzidhulumu nafsi.
Anasema ALLAH (SW) :

{يَا أَيُّهَا الَّذِيْنَ آمَنُوا لاَ تَخُوْنُوا اللهَ وَالرَّسُوْلَ وَتَخُونُوا أَمَانَاتِكُمْ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ} الأنفال 27

“ Enyi Mlioamini ! Msimfanyie khiana ALLAH na Mtume wala msikhini amana zenu na hali mnajua (kuwa haya ni makosa) ”.

Na amesema Mtume (saw) :

((مَا جَلَسَ قَوْمٌ مَجْلِسًا لَمْ يَذْكُرُوا اللهَ فِيْهِ وَلَمْ يُصَلُّوْا عَلَى نَبِيِّهِمْ إِلاَّ كَانَ عَلَيْهِمْ حَسْرَةً))

“ Hawakai watu katika majlisi ikawa hawamtaji ALLAH na hawamsalii Mtume wao isipokuwa watakuwa katika majuto ”.

Enyi Waja wa ALLAH :
Kiongozi wetu, Imamu wetu na mbora wa viumbe Mtume Muhammad (saw) alikuwa akimtaja ALLAH katika hali zake zote, wakati anapokuwa amesimama, amekaa au hata anapolala na kuamka.
Kwani alikuwa anapolala anasema :

((بِاسْمِكَ اللَّهُمَّ أَحْيَا وَأَمُوْتُ))

“ Kwa jina lako (uwezo wako) ewe Mola naishi na nakufa ”.
Na anapoamka husema :

((اَلْحَمْدُ للهِ الَّذِيْ أَحْيَانَا بَعْدَ مَا أَمَاتَنَا وَإِلَيْهِ النُّشُوْرُ))

“ Shukurani zote ni za ALLAH ambae ametupa uhai baada ya kutufisha na marejeo ni kwake yeye ”.

Na ametuusia tuyahuishe majumba yetu kwa kumdhukuru ALLAH kwa wingi na kumuabudu pale aliposema :

((مَثَلُ الْبَيْتِ الَّذِيْ يُذْكَرُ اللهُ فِيْهِ وَالْبَيْتِ الَّذِيْ لاَ يُذْكَرُ اللهُ فِيْهِ مَثَلُ الْحَيِّ وَالْمَيِّتِ))

“ Mfano wa nyumba anayotajwa ALLAH ndani yake na nyumba asiotajwa ALLAH ndani yake ni kama mfano wa aliehai na aliekufa ”.

Enyi Waislamu :
Mcheni ALLAH Mola wenu, muombeni msamaha kutokana na makosa yenu, na mdhukuruni kwa wingi kama alivyokuongoweni, kwani yeye mwenyewe ametuamrisha hayo kwa kusema :

{يَا أَيُّهَا الَّذِيْنَ آمَنُوا اذْكُرُوا اللهَ ذِكْرًا كَثِيْرًا . وَسَبِّحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيْلاً } الأحزاب 41- 42

“ Enyi Mlioamini ! Mdhukuruni ALLAH kwa wingi. Na mtukuzeni asubuhi na jioni ”.

Na jiepusheni na vikao vinavyozungumza mambo ya upuuzi na michezo, kwani mara nyingi mazungumzo katika vikao hivi huwa ni ya uongo, fitna na kusengenya, mambo ambayo ni haramu katika Uislamu.

فَاتَّقُوا اللهَأَيُّهَا الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ، وَاذْكُرُوهُ كَمَا هَدَاكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ .

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَاإِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَىسَيِّدِنَامُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ أَنْ تَرْزُقَ كُلاًّ مِنَّا لِسَانًا صَادِقًا ذَاكِرًا ، وَقَلْبًا خَاشِعًا مُنِيبًا ، وَعَمَلاً صَالِحًا زَاكِيًا ، وَعِلْمًا نَافِعًا رَافِعًا ، وَإِيمَانًا رَاسِخًا ثَابِتًا ، وَيَقِينًا صَادِقًا خَالِصًا ، وَرِزْقًا حَلاَلاً طَيِّبًا وَاسِعًا ، يَا ذَا الْجَلاَلِ وَالإِكْرَامِ.

اَللَّهُمَّ أَعِزَّ الإِسْلاَمَ وَالْمُسْلِمِينَ ، وَوَحِّدِ اللَّهُمَّ صُفُوفَهُمْ ، وَاجْمَعْ كَلِمَتَهُمْ عَلَى الْحَقِّ ، وَاكْسِرْ شَوْكَةَ الظَّالِمِينَ ، وَاكْتُبِ السَّلاَمَ وَالأَمْنَ لِعِبَادِكَ أَجْمَعِينَ .

اَللَّهُمَّ رَبَّنَا اسْقِنَا مِنْ فَيْضِكَ الْمِدْرَارِ ، وَاجْعَلْنَا مِنْ الذَّاكِرِينَ لَكَ فِي اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ، الْمُسْتَغْفِرِينَ لَكَ بِالْعَشِيِّ وَالأَسْحَارِ.

اَللَّهُمَّ أَنْزِلْ عَلَيْنَا مِنْ بَرَكَاتِ السَّمَاءِ ، وَأَخْرِجْ لَنَا مِنْ خَيْرَاتِ الأَرْضِ ، وَبَارِكْ لَنَا فِي ثِمَارِنَا وَزُرُوعِنَا يَا ذَا الْجَلاَلِ وَالإِكْرَامِ .

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ.

رَبَّنَا لاَ تُزِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ رَحْمَةً إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ .

رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنْفُسَنَا وَإِنْ لَمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِيْنَ .

اَللَّهُمَّ اغْفِرْ لِلْمُؤْمِنِينوَالْمُؤْمِنَاتِ ، وَالْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ ، الأَحْيَاءِ مِنْهُمْ وِالأَمْوَاتِ ، إِنَّكَ سَمِيْعٌ قَرِيْبٌ مُجِيْبُ الدَّعَاءِ .

عِبَادَ اللهِ :

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

بسم الله الرحمن الرحيم

الحمدُ لله ربِّ العَالمين، الحمدُ للهِ نحمدُه، ونستعينُه، ونستغفرُه، ونُؤمِنُ به ونَتَوكَّلُ عليه، ونَعُوذُ باللهِ مِنْ شُرورِ أَنْفُسِنا وَمِنْ سَيِّئاتِ أعمالِنا، من يَهْدِهِ اللهُ فلا مُضِلَّ له، ومن يُضلِل فلا هادِيَ له، أشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له، ﴿ ۞ وَعِندَهُۥ مَفَاتِحُ ٱلْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَآ إِلَّا هُوَ ۚ وَيَعْلَمُ مَا فِى ٱلْبَرِّ وَٱلْبَحْرِ ۚ وَمَا تَسْقُطُ مِن وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِى ظُلُمَٰتِ ٱلْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِى كِتَٰبٍ مُّبِينٍ ﴿٥٩﴾ ﴾ ، سُبحَانَك لا عِلْمَ لنا إلا ما عَلَّمتَنَا إنَّكَ أَنْتَ العَلِيمُ الحَكِيمُ، وأشهد أن محمدا عبدُه ورسوله وَصَفِيُّه وخَلِيلُه، أَرْسَلَهُ بالهُدَى ودِينِ الحقِّ لِيُظْهِرَه على الدِّين كُلِّهِ وكفى بالله شهيدا، فَبَلَّغَ الرِّسالةَ وأَدَّى الأَمَانَةَ، ونَصَحَ الأُمَّة وَكَشَفَ اللهُ به الغُمَّةَ، وجاهَدَ في سَبِيلِ دِينه حتّى أتاهُ اليقين ،

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلاً سَدِيداً * يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُم ويغفر لكم ذنوبكم ومن يطع الله ورسوله فقد فاز فوزا عظيما }

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ } الحشر18

أما بعد:

فيا عباد الله: أوصيكم ونفسي بتقوى الله والعملِ بما فيه رضاه.

Enyi waja wa Allah:

Khutba yetu ya leo itagusia kuhusiana na kauli ya Allah mtukufu isemayo:

﴿ وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِۦ عِلْمٌ ۚ إِنَّ ٱلسَّمْعَ وَٱلْبَصَرَ وَٱلْفُؤَادَ كُلُّ أُوْلَٰٓئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْـُٔولًا ﴿٣٦﴾ ﴾ الإسراء: ٣٦

“ Wala usiyafuate usiyo na ujuzi nayo hakika masikio,macho,na moyo,hivyo vyote vitakuja kuulizwa”.

hakika viungo vilivyotajwa katika aya hii, ambavyo ni sikio linalotumika kusikia khabari, na jicho linalotumika katika kuonea, na moyo unaobeba vitu mbali mbali, vyote hivi vilivyotajwa vitakuja kuulizwa kuhusu wewe binaadamu jinsi ulivyovitumia, na hivi viungo ni katika neema kubwa alizotujaalia Allah mtukufu, tukivitumia vizuri viungo hivi basi itakuwa ni sababu ya kupata radhi za Allah na tukivitumia vibaya itakuwa ni sababu ya kutushuhudilia ushahidi mbaya juu yetu, kama Allah alivyosema:

﴿ وَقَالُواْ لِجُلُودِهِمۡ لِمَ شَهِدتُّمۡ عَلَيۡنَاۖ قَالُوٓاْ أَنطَقَنَا ٱللَّهُ ٱلَّذِيٓ أَنطَقَ كُلَّ شَيۡءٖ وَهُوَ خَلَقَكُمۡ أَوَّلَ مَرَّةٖ وَإِلَيۡهِ تُرۡجَعُونَ ٢١ ﴾ فصلت: ٢١

“ **Na wao wataziambia ngozi zao**, **kwa nini mmetushuhudilia**, **nazo zitasema**: **ametutamkisha Allah ambae ametamkisha kila kitu**, **na yeye ndie aliye kuumbeni mara ya kwanza na kwake yeye mtarejea**”.

Kwa dalili hii tumeona kua Allah anao uwezo wa kila kitu, ikiwa yeye ameweza kuitamkisha ngozi izungumze basi anao uwezo wa kuliamrisha sikio, au jicho au moyo kuzungumza, kwa hio tumuogopeni Allah na tuchunge amri zake kikweli,kwa kuwa yote yanayojiri katika fikra zetu,na yanayotamkwa na ndimi zetu,yatapata ushahidi wa kutosha siku ya kiama . Na maana hii inapata nguvu zaidi katika maneno ya Allah yanayosema :

﴿ يَوۡمَ تَشۡهَدُ عَلَيۡهِمۡ أَلۡسِنَتُهُمۡ وَأَيۡدِيهِمۡ وَأَرۡجُلُهُم بِمَا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ ٢٤ ﴾ النور: ٢٤

“**Siku ambayo zitawashuhudia ndimi zao na mikono yao na miguu yao kwa walio kuwa wakiyatenda**” .

Enyi Ndugu waumini:

Kama tunavyoelewa ya kuwa sikio ni Kitu cha mwanzo anacho kitegemea binaadamu katika kupata khabari mbali mbali,lakini pia anaweza akapata khabari kwa kuona,au kusoma katika vyombo vya habari tofauti,na katika mitandao ya kijamii,kwa hivyo ni wajibu wetu kushikama na mfumo tuliofunzwa na dini yetu wa kuchunguza khabari zinazotufikia na kuzichuja ili tuhakikishe ukweli wake kwa sababu ya kuchelea kuja kutumbukia katika mwisho mbaya tukaja tukajutia baadae kwa yale tuliyoyaeneza na kuyasambaza katika khabari za uongo,amesema Allah mtukufu:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِن جَآءَكُمۡ فَاسِقُۢ بِنَبَإٖ فَتَبَيَّنُوٓاْ أَن تُصِيبُواْ قَوۡمَۢا بِجَهَٰلَةٖ فَتُصۡبِحُواْ عَلَىٰ مَا فَعَلۡتُمۡ نَٰدِمِينَ ٦ ﴾ الحجرات: ٦

“ **Enyi mlio amini**, **akikujieni mpotovu na khabari yoyote ichunguzeni**, **msije mkawasibu watu kwa kuto jua**, **na mkawa tena wenye kujuta kwa mliyoyatenda**

.Na mafunzo makubwa tunayojifunza katika aya hii ni kuwa tusifanye haraka ya kutoa hukumu ya kitu au jambo tunaloliona au tunalolisikia mpaka tulithibitishe jambo hilo.Sasa ni wangapi kati yetu wanaingia katika kosa hili kubwa, wanasikia khabari wakazisambaza bila ya kudhithibitisha, au kusoma khabari na kuzisambaza bila ya kuzihakiki, na haya yote leo yamekithiri katika mitandao ya kijamii na katika vyombo vya mawasiliano,amesema mtume (s.a.w):

‘‘Yamtosha mtu kuingia katika dhambi kwa kuhadithia kila anachokisikia’’ .

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ ، أَقُوْلُ قَوْلِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الْكَرِيْمُ .

*** *** ***

الحمدُ لله ربِّ العالمين ، والعاقبة للمتقين ، ولا عدوان إلا على الظالمين ، وأشهد أن لا إله إلا الله ولي الصالحين ، وأشهد أن سيدنا ونبينا محمدا عبده ورسوله ، سيد الأولين والآخرين ، وخاتم النبيين والمرسلين ، صلى الله عليه وسلم وعلى آله وصحبه ، وعلى كل من سار على نهجه إلى يوم الدين .

أما بعد : فيا عباد الله

Enyi waja wa Allah:

Tuna mazingatio makubwa katika uzushi aliozushiwa mama wa waumini bibi Aisha (R.A) pindi alipozushiwa ya kuwa kafanya uchafu na mmoja katika masahaba wa mtume (s.a.w),khabari hizi zilileta taharuki kubwa katika jamii za masahaba,na kukaenea mtafaruki baina yao,lakini kukaibua huzuni na majonzi katika nyoyo za waumini,na hii ndio athari mbaya inayozalika katika tabia hii ya kueneza fitna na khabari zisizo na uhakika,hali hii ilidumu hadi pale Allah alipokuja kumtakasa kwa kushusha aya zinasosomwa katika kitabu chake hadi siku ya mwisho,akataja ndani yake jambo hili baya na kulikemea mno akasema:

﴿ يَعِظُكُمُ ٱللَّهُ أَن تَعُودُواْ لِمِثۡلِهِۦٓ أَبَدًا إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ ١٧ وَيُبَيِّنُ ٱللَّهُ لَكُمُ ٱلۡأٓيَٰتِۚ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ١٨ إِنَّ ٱلَّذِينَ يُحِبُّونَ أَن تَشِيعَ ٱلۡفَٰحِشَةُ فِي ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَهُمۡ عَذَابٌ أَلِيمٞ فِي ٱلدُّنۡيَا وَٱلۡأٓخِرَةِۚ وَٱللَّهُ يَعۡلَمُ وَأَنتُمۡ لَا تَعۡلَمُونَ ١٩ ﴾ النور: ١١ – ١٩

“ … Allah anakuonyeni msirejee tena kufanya kama haya kabisa, ikiwa nyinyi waumini. …Na Allah anakubainisheni aya na Aya, na Allah ni mjuzi mwenye hekima. … Kwa hakika wale wanao penda uenee uchafu kwa walio amini, watapata adhabu chungu katika dunia na akhera, na Allah anajua na nyinyi hamjui”.

Leo tupo katika zama za kuenea mitandao ya kijamii,zama ambazo uaminifu umepungua,uongo umeenea, imekuwa ni wepesi jambo la kusengenyana na kuchonganisha watu kwa kutumia mitandao hiyo au kupeana khabari hasa zile za kuvunja heshima za watu, na jambo hili halifai katika uislamu, mtume Muhammad (s.a.w) amewambia wanaafiki siku moja :

"يا مَعْشَرَ مَنْ آمَنَ بِلِسَانِه وَلَمْ يَدخُلِ الإيمانُ في قَلْبِه، لا تَتَبَّعُوا عَوراتِ المسلمين ولاتُؤْذُوهُم فَإِنَّهُ مَنْ تَتَبَّعَ عَوْرَةَ امْرِئٍ مُسْلِمٍ تَتَبَّعَ اللهُ عَوْرتَه، وَمَنْ تَتَبَعَ اللهُ عَوْرَتَهُ يُفْضِحْهُ اللهُ وَلَوْ فِي جَوفِ دَارِهِ"

“ **Enyi mlioamini kwa kutamka katika ndimi zenu**, **wala haijaingia imani kwenye nyoyo zenu**, **musifatilie aibu za waislamu**, **wala musiwaudhi**, **kwani mwenye kufatilia aibu ya muislamu na allah atazifichua aibu zake**, **na atamfadhehesha hata ikiwa ndani ya nyumba yake** ”.

Enyi waja wa Allah,kwa hio tunatakiwa tuchukuwe tahadhari kubwa ya kuto kuchonganisha watu na kusambaza khabari katika mitandao ya kijamii bila ya kuhakikisha ukweli wake,kwani athari zake ni mbaya katika kuondoa utulivu na amani katika jamii,na kuleta mpasuko na mtengano na kueneza dhana mbaya na kutuhumiana, khasa khasa khabari zinazotufikia katika mitandao ya kijamii, kama vile facebook, twita, whatsapp na mengineyo .

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَاإِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى . اللهم أَعِزَّ الإسلامَ والمسلمين،وأَذِلَّ الشركَ والمشركين، ودَمِّرِ اللّهُمَّ جميعَ أعداءِ الحقِّ والدينِ

"ربنا ءاتنا من لدنك رحمة وهيئ لنا من أمرنا رشدا".

اللهم استخلِفْنَا في أرضِكَ كما استخلفتَ مَنْ قَبْلَنَا من عِبَادَك المُؤْمنين، ومَكِّنْ لَنا دِينَنَا الذي ارتَضَيتَهُ لنا، وأَبْدِلْنَا بِخَوفِنَا أَمْنَا،وبِذُلِّنَا عِزّا،وبِفَقْرِنَا غِنًى، وبِتَشَتُّتِنَا وَحْدَةً، واجْمَعْنا عِلى كلمتك،وألِّفْ بين قُلوبِنا بطاعتك.

اللهم إنَّا ضُعفاءُ فَقَوِّنَا، وإنَّا أذلاءُ فأعِزَّنَا، وإنا فقراء فَأَغْنِنَا ، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام،وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خَلِّصِ المَسجدَ الأقصى وسائرَ بِلادِ المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، وَاجْعَلْهاَ في أيدي عِبادِك المؤمنين،الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار".

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

الرحمة المهداة

بسم الله الرحمن الرحيم

الحمد لله الذي بنعمته تَتمُّ الصالحاتُ، وبالعمل بطاعته تَطيبُ الحياة،وتَنزِلُ البركاتُ،وأشهد أن لا إله إلا اللهُ وحده لا شريكَ له وليُّ الصالحين،وأشهد أن سيدَنا ونبيَّنا وحبيبَنا محمدا عبدُه ورسولُه،أرسله اللهُ بالهدى ودين الحقِّ ليُظهرَه على الدين كلِّه ولو كره المشركونَ،فبلغ الرسالةَ وأدى الأمانةَ ونصح الأمةَ ومحا الظلمةَ وكشف اللهُ به الغمة ،وجاهد في الله حقَّ جهادِه حتى أتاه اليقينُ،فصلوات الله وسلامُه عليه وعلى آله وصحبه والتابعين لهم بإحسان إلى يوم الدين.

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ }

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ علاَّمِ الغيوبِ،فإنها جسرُ النجاةِ من العذاب، والسبيلُ إلى نيلِ الثواب .

Ndugu waislamu:

Kwa hakika ulimwengu kabla ya ujio wa mtume (s.a.w) ulikuwa katika upotofu mkubwa,shirki ilienea,na dhulma ilitawala,na ulimwengu uligubikwa na giza totoro la ujinga na mporomoko wa maadili,ulimwengu ulienea jeuri,uadui,mifarakano na mengi katika maasi na kutoweka tabia njema,Allah ametueleza kuhusu hali hii akasema:

﴿ هُوَ ٱلَّذِى بَعَثَ فِى ٱلْأُمِّيِّـۧنَ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا۟ عَلَيْهِمْ ءَايَـٰتِهِۦ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلْكِتَـٰبَ وَٱلْحِكْمَةَ وَإِن كَانُوا۟ مِن قَبْلُ لَفِى ضَلَـٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٢﴾ ﴾ الجمعة: ٢

"Yeye ndiye aliyempeleka mtume kwenye watu wasiojua kusoma,awasomeshe aya zake na awatakase,na awafunze kitabu na hikma,ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhahiri."

Basi kwa hakika Allah ameukirimu umma huu kwa kumtuma mtume wake Muhammad (s.a.w) aje aumurike ulimwengu kwa nuru ya uislamu,na kuwaongoza waja wa Allah kwenye njia ya haki na uongofu na kuwatoa katika giza la ujinga na kuwapeleka kwenye nuru ya elimu na imani.

Ndugu waumini:

Kwa hakika ujio wake mtume (s.a.w) katika umma huu ni rehma kubwa,inawapasa walimwengu wote kuithamini rehma kubwa hii itokayo kwa ALLAH mtukufu akaitunukia katika umma huu,mtume (s.a.w) ni rehma iliyowaenea viumbe vyote,ni rehma iliyoenea kila chembe iliyoumbwa naALLAH katika ardhi, kuanzia mwanaadamu,majini,wanyama,miti,milima,mawe,na kila kilichopo kwenye ardhi hii,amesema Allah:

﴿ وَمَآ أَرۡسَلۡنَٰكَ إِلَّا رَحۡمَةٗ لِّلۡعَٰلَمِينَ ١٠٧ ﴾ الأنبياء: ١٠٧

“Nasi hatukukutuma ila uwe ni rehma kwa walimwengu wote”.

Na uhakika wa rehma ya mtume (s.a.w) unadhihiri katika maana mbili kuu:

Rehma ya kwanza ni yeye mwenyewe (s.a.w) kwa kuwa alipambwa na Allah kwa tabia ya rehma,na upole,na ulaini wa hali ya juu ya kuweza kuwateka watu na kuvutika nae na hatimae kuukubali utume wake (s.a.w),kwa hakika yeye alikuwa ni rehma kwa masahaba zake kwa kuwa alikuwa na pupa ya kuwavuta katika kheri na hakupenda kuwatia katika mashaka au kuwakalifisha mambo yalio nje ya uwezo wao,naye hukereka pale anapomuona mmoja kati yao anasumbuka na kujitia mashaka na uzito katika sheria za dini,basi aliposikia ya kuwa sahaba mtukufu Othman bin Madh-un (r.a) amezidi mno katika kufanya ibada mpaka kufikia kuvunja haki za watu wake akamwambia:

" أما لك بي أسوةٌ، تصوم النهارَ وتقوم الليلَ، إنَّ لجسدك عليك حقا ولأهلك عليك حقا"

“Je! Hujapata kwangu mimi kigezo chema?!,unafunga michana yote na unasali usiku wote,kwa hakika kiwiliwili chako (nacho) kina haki juu yako,na watu wako pia wana haki juu yako”

Hakika rehma yake ilimuenea pia mwanamke,aliamrisha asitiriwe,na atunzwe na asimamiwe,na afanyiwe wema na upole akasema kuwaagiza waume:

"استَوصُوا بالنساءِ خيرا"

“Jiusieni katika kuwafanyia kheri wanawake”

Na pia alikuwa ni rehma kwa watoto,kwani ametutaka tuwapende na kuwahurumia na kuwachunga na kuwasimamia, na imepokelewa ya kuwa mtume (s.a.w) alikuwa wakati mwengine hukusudia kurefusha sala,lakini husikia kilio cha mtoto katika sala,basi huifupisha sala kwa kuogopea mtoto huyo asijeakamshughulisha mzazi wake”.

Na pia aliwarehemu wazazi wawili kwa sababu ya shida waliyoipata katika kulea na kumsimamia mtoto,akahimiza mno juu ya kuwatii na kuwafanyia ihsani.imesimuliwa ya kuwa **mtume (s.a.w)alijiwa na kijana aliyejawa na furaha katika uso wake kwa kumuunga mkono mtume (s.a.w) ya kuwa atashiriki pamoja naye katika vita,lakini mtume (s.a.w) akamwabia:’Je! Katika wazazi wako yupo aliye hai?,akasema: wote wawili wako hai, akasema mtume (s.a.w):’rejea kwa wazazi wako,na ukakae nao kwa wema na ufanye jihadi (kwa kuwatumikia wao)”**

Na akawahurumia na wanyama pia,akausia wafanyiwe wema wakiwa hai au wakati wanapochinjwa, na akakataza kufanyiwa ubaya na kufanyiwa mateso ,mpaka akafikia kusema;

"دخلتِ امرأةٌ النارَ في هِرَّةٍ ربطتْها فلا هي أطعمتْها ولا هي تركتْها تأكل من خَشَاشِ الأرض"

“Ameingia mwanamke motoni kwa sababu ya paka ambaye alimfungia,basi "hakumlisha wala hakumuacha ale katika majani ya ardhi”.

Basi ndugu yangu muislamu utaona namna gani mtume (s.a.w) alivyoeneza rehma katika ulimwengu, ni rehma iliyowasibu viumbe wote katika dunia, wanyama na majini na mimea na milima na vyenginezo.

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ ، أَقُوْلُ قَوْلِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الْكَرِيْمُ .

*** *** ***

اَلْحَمْدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ، وَلاَ عُدْوَانَ إِلاَّ عَلَى الظَّالِمِينَ . وَنَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ وَلِيُّ الصَّالِحِينَ ، وَنَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ إِمَامُ الأَنْبِيَاءِ وَالْمُرْسَلِينَ ، وَأَفْضَلُ خَلْقِ اللهِ أَجْمَعِينَ ، صَلَوَاتُ اللهِ وَسَلاَمُهُ عَلَيْهِ ، وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَالتَّابِعِينَ لَهُمْ بِإِحْسَانٍ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عَبَادَ اللهِ :

Enyi ndugu waumini:

Ama maana nyengine ya rehma inayodhihiri kwa bwana mtume (s.a.w) kwa umma huu ni sheria tukufu aliyokuja nayo, kwani kwa hakika sheria ya kiislamu ni sheria nyepesi,iliyobeba misingi madhubuti inayoendana na hali halisi za viumbe,na kuchunga dhurufu za mwanaadamu,ni sheria iliyojengeka katika msingi wa kuondoa uzito na shida kwa mwanaadamu katika nyanja zake zote,sawa ni katika mambo ya kiibada au katika mambo ya muamala baina ya mtu na watu wengine,amesema Allah mtukufu;

﴿ وَمَا جَعَلَ عَلَيۡكُمۡ فِي ٱلدِّينِ مِنۡ حَرَجٖۚ ﴾ الحج: ٧٨

“Na wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini”

Na akasema mtume (s.a.w):

"الدينُ يُسرٌ ولن يُشادَّ الدينَ أحدٌ إلا غلبَه..."

“Dini ni nyepesi,na hakuna yoyote atakaeikazia dini isipokuwa itamshinda…”

Kwa hio mtume (s.a.w) ni rehma kubwa ilitunukiwa katika umma huu tangu kuja kwake mpaka kuondoka kwake duniani,na haitowacha sheria yake kumurika katika dunia,na kutoa mafunzo na maelekezo kwa wanaadamu hadi Allah atakapoirithi ardhi na vilivyomo katika ardhi.

Ni juu yetu kumtukuza mtume Muhammad (s.a.w) na kufuata mwenendo wake wote na kushikamana na maagizo yake,na kukamatana na sunna

yake,na kujifunza sira yake, na kupandikiza mapenzi yake kwa kizazi cha kiislamu, na kumtangazia katika ulimwengu na kumhami na kuinusuru dini yake,kwani hapo ndio hupatikana kufuzu na kufaulu mbele ya Allah,amesema Allah:

﴿ فَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِهِۦ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَٱتَّبَعُواْ ٱلنُّورَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ مَعَهُۥٓ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ﴿١٥٧﴾ ﴾

الأعراف: ١٥٧

"Basi waliomuamini yeye,na wakamhishimu,na wakamsaidia,na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye,hao ndio wenye kufanikiwa".

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَاإِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى .

للهم أَعِزَّ الإسلامَ والمسلمين،وأَذِلَّ الشركَ والمشركين، ودَمِّرِ اللّهُمَّ جميعَ أعداءِ الحقِّ والدينِ .

"ربنا ءاتنا من لدنك رحمة وهيئ لنا من أمرنا رشدا".

اللهم استَخلِفْنَا في أرضِكَ كما استخلفتَ مَنْ قَبْلَنَا من عِبَادَكَ المؤْمِنينَ، ومَكِّنْ لَنا دِينَنَا الذي ارتَضَيتَهُ لنا، وأَبْدِلْنَا بِخَوفِنَا أَمْنَا،وبِذُلِّنَا عِزّا،وبِفَقْرِنَا غِنًى، وبِتَشَتُّتِنَا وَحْدَةً، واجْمَعْنا عِلى كلمتك،وألِّفْ بين قُلوبِنا بطاعتك.

اللهم إنَّا ضُعفاءُ فَقَوِّنَا، وإنَّا أذلاءُ فأعِزَّنَا، وإنا فقراء فَأَغْنِنَا ، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام،وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خَلِّصِ المِسجدَ الأقصى وسائرَ بِلادِ المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، وَاجْعَلْهاَ في أيدي عِبادِك المؤمنين،الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار".

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

بسم الله الرحمن الرحيم

الحمدُ لله الذي جعلَ الإيمانَ لِعبادِهِ المؤمنين أَمْناً ، وآتَى عبادَهُ مِن رِزقه فَضْلاً ومَنًّا ، سُبحانه خلقَ الأمانةَ وحرَّمَ الخيانةَ ، أحمدُه بما هو له أهل من الحمدِ وأُثني عَلَيْه ، وأستغفره مِنْ جميعِ الذنوب وأَتوبُ إليه ، وأومنُ به وأتوَكلُ عليه ، من يَهْدِهِ اللهُ فلا مُضِلّ لَه ، وَمَن يُضلل فلا هادي لَه ، وأشهدُ أن لا إله إلا الله وحده لا شريكَ له ، من يُطع اللهَ ورسولَه فقد رَشَدَ ، ﴿ وَمَن يَعْصِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾ ﴾ الأحزاب: ٣٦

وأشهد أن سيدنا ونبيَّنا محمداً عبدُه ورسولُه ، وصفيُّه وخلِيلُه ، بلَّغَ الرِّسالة وأدَّى الأمانةَ ، ونصح الأمّة ، وكشف الغمّة ، اللهمّ صلِّ وسلِّم على نبيِّنا محمَّدٍ وعلى آل محمد ، كما صليت وسَلَّمتَ على إبراهيم وعلى آل إبراهيم ، إنك حَميدٌ مَجيدٌ ، وباركْ على محمد وعلى آل محمد كما باركت على إبراهيم وعلى آل إبراهيم ، إنك حميد مجيد .

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلاً سَدِيداً * يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُم ويغفر لكم ذنوبكم ومن يطع الله ورسوله

فقد فاز فوزا عظيما }

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ } الحشر18

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ ،فاتقوا الله تعالى حق التقوى، والتزموا شريعته المثلى،ولا تركنوا إلى الشيطان والهوى .

Enyi waja wa ALLAH ,

Muogopeni ALLAH mtukufu , na tambueni ya kuwa ALLAH mtukufu alikadimisha amana kwa mbigu na ardhi na milima , na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa , lakini mwanaadamu akakubali kuibeba amana hiyo , hakika yeye mwanaadamu amekua dhalimu wa nafsi yake na mjinga sana kwa kubeba amana nzito halafu asiweze kuitekelezea haki yake ,amana kubwa hii ya kusimamia majukumu ya kisheria na kuendesha ukhalifa katika hii ardhi kwa kuimarisha na kuleta ustaarabu na kueneza maadili mema ,na kuondoa kila uharibifu na ufisadi katika ardhi,ni amana nzito hio aliyoitundika ALLAH mtukufu katika shingo ya mwanaadamu , amesema ALLAH mtukufu :

﴿ وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَٰٓئِكَةِ إِنِّى جَاعِلٌ فِى ٱلْأَرْضِ خَلِيفَةً ۖ قَالُوٓاْ أَتَجْعَلُ فِيهَا مَن يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ ٱلدِّمَآءَ وَنَحْنُ نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ ۖ قَالَ إِنِّىٓ أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾ ﴾ البقرة: ٣٠

“ Na pale mola wako mlezi alipo wambia malaika : mimi nitamueka katika ardhi khalifa (mfwatizi) , wakasema : utaweka humo atakaefanya uharibifu humo na kumwaga damu , hali sisi tunakutakasa kwa sifa zako na tunakutaja kwa utakatifu wako ? akasema : hakika mimi nayajua musio yajua ”

Na asili katika amana ni kutekeleza haki na kusimamisha mambo ya wajibu yote kwa ujumla,hii inamaanisha ya kuwa maana ya amana haikufungwa katika kuhifadhi mali za watu peke yake,bali kila ambacho ulichotakiwa ukisimamie ni katika amana na utakwenda kuulizwa mbele ya Allah,basi mke ni amana,watoto ni amana,sala ni amana,kuifikisha dini ya Allah ni amana,kutunza heshima ni amana ,na pia kuhifadhi siri ni amana, kwa hiyo mtu mwenye kuchukuwa amana yoyote anatakiwa awe mlinzi wa nafsi yake , na ajue kuwa ALLAH anamchunga katika kila jambo lake analolifanya .asijaribu kabisa kumfanyia khiyana mola wake katika amana aliyombebesha, amesema ALLAH mtukufu :

﴿ وَكَانَ ٱللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ رَّقِيبٗا ٥٢ ﴾ الأحزاب: ٥٢ “ Na ALLAH anakichunga kila kitu ”

Hakika sifa ya kubeba amana, inampelekea mtu ahisi uzito wa majukumu, na amuonee haya ALLAH mtukufu anayemchunga na kujua kila siri yake na dhahiri yake,hii humpelekea kuweza kutekeleza yote katika haki za ALLAH , katika hali zote , na vile vile kwa upande wa viumbe wenziwe atajitahidi kuwatekelezea na kuzihifadhi haki zao .

Ndugu waislamu;

Allah mtukufu ameamrisha waja wake wahifadhi amana , akasema :

﴿ ۞ إِنَّ ٱللَّهَ يَأۡمُرُكُمۡ أَن تُؤَدُّواْ ٱلۡأَمَٰنَٰتِ إِلَىٰٓ أَهۡلِهَا وَإِذَا حَكَمۡتُم بَيۡنَ ٱلنَّاسِ أَن تَحۡكُمُواْ بِٱلۡعَدۡلِۚ إِنَّ ٱللَّهَ نِعِمَّا يَعِظُكُم بِهِۦٓۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ سَمِيعَۢا بَصِيرٗا ٥٨ ﴾ النساء: ٥٨

“ Hakika ALLAH anakuamrisheni muzirudishe amana kwa wenyewe . na mnapo hukumu baina ya watu muhukumu kwa uwadilifu . hakika haya anayokuwaidhini ALLAH ni mazuri sana . hakika ALLAH ndie mwenye kusikia , mwenye kuona . ”

Na mtume (s.a.w) akamvua imani muislamu ambaye hatekelezi amana, akasema (s.a.w) :

" لا إيْمَانَ لِمَنْ لَا أَمانةَ لَهُ " **" Hana imani Yule ambae hatekelezi amana "**

Na mtu huyu amestahiki sifa hii ya kuwa hana imani kwa sababu ya kupoteza amana,na yule anaepoteza amana basi anapoteza kila kitu , anapoteza mambo ya wajibu na kuvuka mipaka , na kufanya yaliokuwa ya haramu , na kukosa tabia njema , kwa ajili hiyo huenea ufisadi ,dhulma,khiyana katika jamii,kwa sababu tu ya kukosekana amana .

Kwa hakika kutoweka kwa amana katika jamii ni kiashirio kibaya cha kuondokewa na rehma ya Allah,na kuenea fitna na majanga katika ulimwengu,amana itakapopuuzwa ni dalili ya kukaribia kiama, kwani mtume Muhammad (s.a.w) amesema :

" إذا ضيِّعتِ الأمانةُ فانتَظرِ الساعةَ "

" Itakapo potezwa amana basi subiri kiama "

فَسُئِلَ عَن تَضْعِيْيهَا فَقَالَ : " أَنْ يُوسَّدَ الأمرُ إلَى غيرِ أَهلِهِ "

Akaulizwa mtume (s.a w) jinsi ya kuipoteza, akasema : “ Ni kuegemezwa jambo (uongozi) kwa watu wasiostahiki ” .

Kwa hio anatakiwa mwanadamu awe muaminifu wa nafsi yake , na heshima yake , na vyote vilivyofungamana na yeye , yeye kachukuwa jukumu juu ya hayo yote mbele ya mola wake ,na Allah mtukufu amesema :

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَخُونُواْ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَ وَتَخُونُوٓاْ أَمَٰنَٰتِكُمۡ وَأَنتُمۡ تَعۡلَمُونَ ٢٧ ﴾ الأنفال: ٢٧

“ Enyi mlio amini ! msimfanyie khiyana ALLAH na mtume , wala msikhini amana zenu nanyi mnajua ”

Hakika binaadamu anaweza kumfanyia khiyana ALLAH kwa kupuuza maamrisho yake , na anaweza kumfanyia khiyana mtume (s.a.w) kwa kuwacha maagizo yake , na vile vile anaweza kuzifanyia khiyana amana za watua kwa kutozichunga ,na kuzizembea bila ya kuzihifadhi.

Enyi waumini :

Hakika katika Amana kubwa kwa muislamu ni kuaminiwa katika kusimamia majukumu ya waja wa ALLAH , kwa aina yoyote ya majukumu yatakavyokuwa , sawa ikiwa ni majukumu ya kuwasimamia wadogo ama wakubwa , wanawake au wanaume, basi anatakiwa afanye wajibu wake wa kuchunga amana hizo, wala asizipoteze . kwani imepokewa kutoka kwa mtume (s. a. w) amesema :

" كفَى بِالمَرءِ إثمًا أنْ يُضَيِّعَ مَنْ يَعُولُ "

“ Inatosha kupata dhambi kwa mtu kwa kutowashughulikia wale anaowasimamia ”

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ ، أَقُوْلُ قَولِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الرَّحِيْمُ.

*** *** ***

الحمدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ، وَلاَ عُدْوَانَ إِلاَّ عَلَى الظَّالِمِينَ . وَنَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ وَلِيُّ الصَّالِحِينَ ، وَنَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ إِمَامُ الأَنْبِيَاءِ وَالْمُرْسَلِينَ ، وَأَفْضَلُ خَلْقِ اللهِ أَجْمَعِينَ ، صَلَوَاتُ اللهِ وَسَلاَمُهُ عَلَيْهِ ، وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَالتَّابِعِينَ لَهُمْ بِإِحْسَانٍ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عَبَادَ اللهِ :

Enyi waja wa ALLAH:

إِنَّ أَمانَةَ الأموالِ أَمانةٌ عظيمةٌ وعَلى الناسِ أن يتقُو اللهَ تَعَالى فِي ذلك

Hakika amana ya kuhifadhi mali ni amana kubwa , basi watu wamuogope mola wao katika hilo .

Watu wangapi wameaminiwa kuhifadhi amana ya mali na hawakuweza kuhifadhi , na wala hawakuweza kuzirejesha kama zilivyo kwa watu wake.Na wangapi wamechukua madeni kwa watu na hawakuweza kurejesha walichokikopa kwa watu hao , au mwengine anachukuwa ahadi atarejesha wakati maalumu ,lakini anapuuza na kuzembea kurejesha bila ya sababu ya msingi . na kufanya hayo kwa hakika ni dhulma , anasema mtume (s,a,w)

"مَطْلُ الغَنِيِّ ظُلْمٌ "

" Kuchelewesha deni tajiri ni dhulma "

Na watu wangapi wamenunua bidhaa za watu hawakuweza kuwatimizia haki zao ! .

Na yule ambae ameajiriwa kazi na akawa haitekelezei haki yake basi pia anahisabika kuwa amaeipoteza amana, bali amefanya khiyana, Allah mtukufu atukinge na hayo. Na binaadamu awe muaminifu katika mali yake , asiitumue isipokuwa katika mambo ya kheri na wala asiitumie katika mambo ya shari na haramu , atakapoitumia katika haramu basi pia atakuwa ameifanyia khiyana amana , vipi aitumie katika haramu na ALLAH mtukufu amemuamrisha ashukuru neema ?!

Basi watu wanatakiwa wamuogope ALAH mtukufu , na wasimamie amana zao , watakuja kuulizwa kutokana na amana hizo mbele ya ALLAH mtukufu .

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَاإِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

للهم أَعِزَّ الإسلامَ والمسلمين،وأَذِلَّ الشركَ والمشركين، ودَمِّرِ اللّهُمَّ جميعَ أعداءِ الحقِّ والدينِ .

اللهم استَخلِفْنَا في أرضِكَ كما استخلفتَ مَنْ قَبْلَنَا من عِبَادِكَ المُؤْمِنينَ، ومَكِّنْ لَنا دِينَنَا الذي ارتَضَيتَهُ لنا، وأَبْدِلْنَا بِخَوفِنَا أَمْنَا،وبِذُلِّنَا عِزّا،وبِفَقْرِنَا غِنًى، وبِتَشَتُّتِنَا وَحْدَةً، واجْمَعْنا عِلى كلمتك،وألِّفْ بين قُلوبِنا بطاعتك.

اللهم إنَّا ضُعفاءُ فَقَوِّنَا، وإنَّا أذلاءُ فأعِزَّنَا، وإنا فقراء فَأَغْنِنَا ، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام،وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خَلِّصِ المَسجدَ الأقصى وسائرَ بِلادِ المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، وَاجْعَلْهاَ في أيدي عِبادِك المؤمنين،الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار".

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ

ذوالقعدة **خذوا حذركم من المضار**

الحمدُ للهِ الذي جعلَ لنا في الطيباتِ صِحةَ الأبدانِ وراحةَ الجَنانِ، وأشهد ان لا إله إلا اللهُ وحده لا شريكَ له، حَضَّ على حِفظِ النفسِ مِنَ الأَدْرانِ، ومَنَعَ كلَّ ما كان مُنافيًا لِسلوكِ الإيمانِ، وأشهد أن محمدا عبدُ اللهِ ورسولُه، أقربُ الناسِ إلى الله منزلةً وشأنا، صلى الله وسلم عليه وعلى آله وصحبه وتابعيه أولِي العلمِ والنُّهىَ.

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ }

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ علاَّمِ الغيوبِ،فإنها جسرُ النجاةِ من العذاب، والسبيلُ إلى نيلِ الثواب .

Ndugu waislamu:

Tambueni ya kuwa Allah mtukufu amemfadhilisha mwanaadamu na akamkirimu takrima kubwa,na akamrahisishia njia za kupata manufaa yote anayoyahitajia kupitia ardhini au mbinguni,na akamruhusu kunufaika na rizki zote za halali,lakini Allah akamtaka mwanaadamu huyo asile wala asinywe isipokuwa kizuri chenye manufaa,na asikaribiye vibaya vyote vyenye madhara juu yake,haya ndio mafunzo ya mola wetu katika kitabu chake kitukufu,na ndio maelekezo ya mtume wake (s.a.w),akasema Allah mtukufu:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ كُلُواْ مِمَّا فِي ٱلۡأَرۡضِ حَلَٰلٗا طَيِّبٗا وَلَا تَتَّبِعُواْ خُطُوَٰتِ ٱلشَّيۡطَٰنِۚ إِنَّهُۥ لَكُمۡ عَدُوّٞ مُّبِينٌ " ١٦٨ إِنَّمَا يَأۡمُرُكُم بِٱلسُّوٓءِ وَٱلۡفَحۡشَآءِ وَأَن تَقُولُواْ عَلَى ٱللَّهِ مَا لَا تَعۡلَمُونَ ١٦٩ ﴾

”Enyi watu,kuleni vilivyomo katika ardhi ,halali na vizuri,wala musifuate nyayo za shetani,hakika yeye ni adui wenu aliye wazi.Hakika si chochote,yeye anakuamrisheni maovu na machafu na kumsingizia Allah yale musiyoyajua”.

Kwa hivyo inampasa mwanaadamu aepuke kila kinachodhuru afya yake,na kumuondolea uzima wake,sawa iwe ni chakula au kinywaji,au chochote ambacho utumiaji wake utampelekea matatizo katika afya yake,kama uvutaji wa sigara kwa aina zake zote,sawa ikiwa ni sigara au shisha au hizi sigara za kisasa zinazoitwa sigara za electronic,au chochote kinacholewesha au kuondoa akili,kwani kwa hakika imebainika khatari ya uvutaji sigara kwa kila mwenye akili, sigara ni shari tupu,,na taathira yake katika mifumo ya mwili wa mwanaadamu ni kubwa mno,na maradhi yanayosababishwa na sigara ni mengi

na mabaya sana,kama vile kensa ya mapafu,kensa ya koo,kensa ya kibofu cha mkojo,na madhara makubwa katika mfumo wa umengenyaji wa chakula,na mfumo wa damu,na wameeleza madaktari kuwa sigara inaweza kumsababishia mtu utasa (kukosa kizazi) ,na kuharakiwa na uzee,na imethibiti katika tafiti za kitaalamu ya kuwa watu wasiopungua milioni na nusu wanakufa ulimwenguni kila mwaka kwa janga la sigara,kwa hio sigara ni kitu kinachouwa pole pole,inampasa mtu kutahadhari na janga hili,amesema Allah mtukufu:

﴿ وَلَا تَقۡتُلُوٓاْ أَنفُسَكُمۡۚ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ بِكُمۡ رَحِيمٗا ٢٩ ﴾ النساء: ٢٩

“Na wala musiuwe nafsi zenu,hakika Allah ni mwingi wa kukuhurumieni”.

Na pia amesema Allah mtukufu katika kitabu chake:

﴿ وَأَنفِقُواْ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ وَلَا تُلۡقُواْ بِأَيۡدِيكُمۡ إِلَى ٱلتَّهۡلُكَةِۛ وَأَحۡسِنُوٓاْۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلۡمُحۡسِنِينَ ١٩٥ ﴾ البقرة: ١٩٥“

“Na toeni katika njia ya Allah na wala musijiingize kwa mikono yenu kwenye maangamizi,na mufanye wema,hakika Allah anawapenda wanaofanya wema”.

Ndugu waumini:

Allah ameharamisha kwa mwanaadamu kila kibaya au kichafu ambacho kinaleta madhara katika siha yake, akasema Allah:

﴿ ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِيَّ ٱلۡأُمِّيَّ ٱلَّذِي يَجِدُونَهُۥ مَكۡتُوبًا عِندَهُمۡ فِي ٱلتَّوۡرَىٰةِ وَٱلۡإِنجِيلِ “ يَأۡمُرُهُم بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَيَنۡهَىٰهُمۡ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡخَبَٰٓئِثَ وَيَضَعُ عَنۡهُمۡ إِصۡرَهُمۡ وَٱلۡأَغۡلَٰلَ ٱلَّتِي كَانَتۡ عَلَيۡهِمۡۚ فَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِهِۦ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَٱتَّبَعُواْ ٱلنُّورَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ مَعَهُۥٓ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ ﴾ الأعراف: ١٥٧

”Ambao wanaomfata mtume ,nabii,asiyesoma wala kuandika,wanamkuta kaandikwa kwao katika taurati na Injili,anayewaamrisha mema,na anawakataza maovu,na anawahalalishia vizuri,na anawaharamishia vibaya,na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao,basi wale waliomuamini yeye ,na wakamuheshimu,na wakamsaidia,na wakaifuata nuru iliyoteremshwa Pamoja naye,hao ndio wenye kufanikiwa”.

Ama tukija kuangalia chanzo cha madhara haya yaliyomo katika sigara ,kwanza ni mti wenyewe wa sigara umesheheheni mada zenye madhara mabaya kwa mwanaadamu,kama naykotiin ambayo huteketeza katika mapafu na huathiri katika mfumo wa damu,na cabondixide,pamoja na mada za cemical zinazozidishwa na wale wanaotenegeneza kitu hichi,isitoshe kuna madhara ya kiuchumi yanayosababishwa na janga hili,kuanzia ile mali inayopotea kununulia viboksi vya sigara,na mali ambayo atakuja kuitoa mbeleni kwa ajili ya kujitibu kwa maradhi yatakayosababishwa na janga hili,lakini na mali nyingi zinazotolewa na serikali kwa kuwasaidia hawa waathirika wa janga hili,watu hawa ambao ilitakiwa wawe ni msaada wa kujenga taifa badala yake wamekuwa ni mzigo kwa taifa.

فاتقوا الله عبادَ اللهِ -واحفظوا أَنفسَكم مِن كلِّ ما يَضرُّ أَبدانَكم وعقولَكم، واشكروا نعمتَ اللهِ إن كنتم إياه تعبدونَ.

****

الحمد لله الذي حرَّم على عبادِه الخبائثَ، وأحل لهم الطيباتِ،وجعلَ على هُداهُ دلائلَ وعلاماتِ،وأشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له،رفيعُ الدرجاتِ، وأشهد أن سيدنا ونبينا محمدا عبده ورسوله المبعوثُ مبشرا ومُنذِرا بالآيات،وعلى آله وصحبه ، ومن سار على دربِه إلى يوم يُقسم الناس إلى فريقينِ إلى السعيرِ وإلى الجَنَّاتِ.

أما بعد:

Ndugu waislamu:

Lau mmoja wetu angetakiwa auze nafsi yake kwa thamani iliyo ghali,au apewe vyote vya duniani ili auze nafsi yake basi bila shaka angekataa kata kata,basi ni kwanini baadhi yetu tunakubali kuziuza nafsi zetu kwa bei rahisi mno,mtu hahisi uzito kuuwa nafsi yake kwa kutumia madawa ya kulevya,tumbaku,sigara,mirungi na mengineo,kwa hakika hizi ni kama bastola ambazo mtu anazitumia kujiangamiza mwenyewe kwa mkono wake na kwa pesa yake.

Ndugu zangu katika Imani:

Haijifichi kwenu ya kuwa idadi ya wanaovuta sigara na wanaosibiwa na uraibu wa kutumia vilevi ni yenye kuzidi mwaka baada ya mwaka,na zimekuwa sigara za electronic mikononi mwa vijana na wasichana,bali mpaka wanafunzi wa vyuo

au wa shule wamekosa haya ya kuwazuiya kuchukua vitu hivi katika vyuo,basi ni wajibu wetu wazazi ,na viongozi,kumcha Allah katika amana ambayo Allah ametubebesha, tuwaongoze vijana wetu njia iliyo sawa,na tuwaepushe kutokana na maovu yenye kuleta maangamizi ya dunia na akhera,amesema Allah mtukufu:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ قُوٓاْ أَنفُسَكُمۡ وَأَهۡلِيكُمۡ نَارٗا وَقُودُهَا ٱلنَّاسُ وَٱلۡحِجَارَةُ عَلَيۡهَا مَلَٰٓئِكَةٌ غِلَاظٞ شِدَادٞ لَّا يَعۡصُونَ ٱللَّهَ مَآ أَمَرَهُمۡ وَيَفۡعَلُونَ مَا يُؤۡمَرُونَ ٦ ﴾ التحريم: ٦

“Enyi mlioamini,ziokoeni nafsi zenu na watu wenu kutokana na moto,kuni zake ni wat una mawe ,juu yake kuna Malaika wenye nguvu,wakali,hawamuasi Allah kwa yale aliyowaamrisha,na wanatekeleza yale wanayoamrishwa”.

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَاإِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى . اللهم أَعِزَّ الإسلامَ والمسلمين،وأَذِلَّ الشركَ والمشركين، ودَمِّرِ اللّهُمَّ جميعَ أعداءِ الحقِّ والدينِ .

"ربنا ءاتنا من لدنك رحمة وهيئ لنا من أمرنا رشدا".

اللهم استخلِفْنَا في أرضِكَ كما استخلفتَ مَنْ قَبْلَنَا من عِبَادَك المُؤْمِنينَ، ومَكِّنْ لَنا دِينَنَا الذي ارتَضَيتَهُ لنا، وأَبْدِلْنَا بِخَوفِنَا أَمْنَا،وبِذُلِّنَا عِزّا،وبِفَقْرِنَا غِنًى، وبِتَشَتُّتِنَا وَحْدَةً، واجْمَعْنا عِلى كلمتك،وألِّفْ بين قُلوبِنا بطاعتك.

اللهم إنَّا ضُعفاءُ فَقَوِّنَا، وإنَّا أذلاءُ فأعِزَنَا، وإنا فقراء فَأَغْنِنَا ، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام،وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خَلِّصِ المَسجدَ الأقصى وسائرَ بِلادِ المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، وَاجْعَلْهاَ في أيدي عِبادِك المؤمنين،الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار".

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

في ذكر المولد

بسم الله الرّحمن الرّحيم .

الحمدُ لله ربّ العالمين ، أَكْرَمَنا بالإسلامِ , وامتنَّ علينا بنعمةِ الإيمان وبَعثَ رَسولَه – عليه الصلاةُ والسلامُ – أَحمدُه سبحانه بما هُو له أهلٌ من الحمدِ وأُثني عَلَيه ، وأُومنُ به وأَتوكلُ عَلَيه ، من يهده الله فلا مضلَّ له ، ومن يُضللْ فلا هاديَ له . وأشهد أن لا إله إلاّ اللهُ وحده لا شريكَ له ، أرسل رسولَه الكريمَ لِيَهْديَ الناسَ بإذنِ ربِّه إلى صراطٍ مستقيمٍ , وأشهد أنّ سيّدَنا ونبيّنا محمداً عبدُه ورسولُه ، البشيرُ النذيرُ والسراجُ المنيرُ , الوفيُّ البارُّ , أسوةُ كلِّ شاكرٍ وصبَّارٍ ,صلى الله عليه وسلّم وعلى آله وصحبِه ، وعلى كلّ من اهتدى بهديِه واستنّ بسنّته إلى يوم الدّين .

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلاً سَدِيداً * يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُم ويغفر لكم ذنوبكم ومن يطع الله ورسوله فقد فاز فوزا عظيما }

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ } الحشر18

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ ،فاتقوا الله تعالى حق التقوى، والتزموا شريعته المثلى،ولا تَركَنُوا إلى الشيطان والهَوَى .

Enyi waja wa ALLAH :

Tambueni ya kuwa ALLAH amewaneemesha waja wake waumini kwa neema mbili kubwa , neema ya kwanza ni neema ya imani kwa kumuamini Allah na kusadikisha yale yote aliyotuelezea kupitia wahyi wa kitabu chake kitukufu cha qur-ani na wahyi wa sunna ya mtume wake Muhammad (s.a.w), amesema Allah mtukufu katika kuonesha uzito wa neema hii :

{يَمُنُّونَ عَلَيْكَ أَنْ أَسْلَمُوا قُلْ لَا تَمُنُّوا عَلَيَّ إِسْلَامَكُمْ بَلِ اللَّهُ يَمُنُّ عَلَيْكُمْ أَنْ هَدَاكُمْ لِلْإِيمَانِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ }

الحجرات: 17

[Wanakusimbulia kuwa wamesilimu! Sema: Msinisimbulie kwa kusilimu kwenu. Bali Mwenyezi Mungu ndiye aliye kufanyieni hisani kwa kukuongoeni kwenye Imani, ikiwa nyinyi ni wakweli.]

Ama neema ya pili ni neema ya kutumwa katika umma huu mtume Muhammad (s.a.w),kwa ajili ya kuondoa upotofu na kuwatoa watu katika

viza vya ujinga na maasi kuwapeleka kwenye nuru ya elimu na kumtii Allah,aliletwa kwa ajili ya kuwatanabahisha walioghafilika,na kuwaamsha waliolala,na kuwaongoa waliopotoka na kuwaelekeza waliokuwa watumwa wa matamanio yao na nafsi zao,basi ni ukubwa ulioje huu wa neema ya ujio wa mtume (s.a.w) anatueleza ALLAH kuhusu neema hii:

{{لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْ أَنْفُسِهِمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلُ لَفِي ضَلَالٍ مُبِينٍ}} [آل عمران: 164

[Hakika Mwenyezi Mungu amewafanyia wema mkubwa Waumini vile alivyo waletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe, anaye wasomea Aya zake, na anawatakasa, na anawafunza Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya hapo walikuwa katika upotovu ulio wazi.]

Kwa hakika mazazi ya mtume Muhammad (s.a.w) ni tukio kubwa katika historia ya waislamu,na kupewa kwake utume ulikuwa ni mabadiliko makubwa katika tarekhe ya ulimwengu , na baina ya mazazi yake na kupewa kwake utume aliishi muda usio pungua miaka arubaini , waliokua wakiishi nae katika kipindi hicho walishuhudia tabia zake njema na sifa nzuri alizo nazo , walikua nae tangu kijana mdogo akishirikiana na vijana wenziwe kufanya kazi , na walimshuhudia alipokua mtu mzima walipomchagua hakimu baina yao , akaweza kuondoa tofauti zao, na akapatanisha waliogombana wakaelewana. .

Enyi ndugu waislamu :

Ilikua kutumwa kwa mtume(s.a.w) ni alama ya kuanza maisha mapya ,na kupambazuka asubuhi ya ushindi wa haqi juu ya batili na ushindi wa wapenzi wa Allah juu ya wafuasi wa shetani, kwa hakika kuna wengi katika watu wenye akili na busara waliokua wanasubiri kwa hamu ipambazuke asubuhi hio, kwa kua walikuwa wamechoshwa kutokana na dhulma na giza la shirki na maasi lililotapakaa katika jamii ,akatumwa bwana wa viumbe Muhammad (s.a.w),akatakasa nafsi zilizokufa na akaweza kuzihuisha na kuzifanya zilainike na zijae mapenzi ya Allah , kwa kweli amelingania watu katika kila kheri kwa kuwa Mola wake amemchagua na kumuandaa kwa kazi hio ,na akamsifu kwa kusema :

{{وَإِنَّكَ لَعَلَى خُلُقٍ عَظِيمٍ}} [القلم: 4

[[Na hakika wewe una tabia tukufu.]]

Ndugu waumini:

Ujumbe mkubwa aliokuja nao mtume(s.a.w) ni tabia njema,na ndio maana Allah hakumsifu kwa sura yake wala umbile lake zuri,lakini alimsifu kwa tabia zake, mtume (s.a.w) alifika kilele katika tabia njema,alikuwa mwepesi kwa watu,mlaini wa tabia ,akiwashajiisha watu na akiwapa matumaini, hakuwa mgumu kwa watu, ,na alikuwa akisema :

{{يَسِّروا ولا تُعَسِّروا وبَشِّروا ولا تُنفِّروا}}

[[Fanyeni wepesi na wala musiwakwaze watu , na wapeni moyo wala musiwakatishe tamaa]] , alikua anamshukuru mola wake kwa kila neema aliyomjaalia ,na kila asubuhi akimuomba kwa kusema:

((اللَّهُمَّ مَا أَصْبَحَ بِي مِن نعْمَةٍ ، أو بأحدٍ من خَلْقِكَ ، فَإِنَّها مِنْكَ وحدَكَ ، لا شَريكَ لَكَ ، لَكَ الحمدُ))

"Ewe mola wangu,chochote kitakachopambazuka kwangu katika neema au kwa yoyote katika viumbe vyako,basi kwa hakika neema hio inatokana na wewe peke yako,huna mshirika,na sifa njema zote ni za kwako".

Alikua mtume (s.a.w) anamuanza kwa salamu kila anayemkuta , na haachi kua mwenye kutabasamu kwa watu , na anaanza kumpa mkono kila anaemsalimia , anamkirimu anayeingia kwenye nyumba yake , na alikua akiwaita watu kwa majina wanayo yapenda kwa lengo la kutia mapenzi baina yao .

Enyi waja wa ALLAH :

Hakika mwenye kusoma vizuri historia ya mtume , lazima atakiri ya kuwa mtume (s.a.w) kwa muda mchache alioishi katika umri wake,Allah alimuwafikisha kueneza mazuri mengi katika ulimwengu,na akaweza kusimamisha uadilifu,na kusimamisha dola ,na akafanikiwa kuwaathiri wengi kwa tabia zake njema na hatime wakamkubali na kuupokea vizuri ujumbe aliokuja nao,akaeneza salama na amani katika dunia , na mapenzi na umoja , na kuheshimiana na kushikamana ,hakuna mwenye kufanya kiburi wala kufanya jeuri kwa wenziwe,bali wote wakawa ni sawa kama meno ya shanuo,aliwausia watu kwa kusema :

[[Hakika ALLAH amenifunulia nikwambieni ya kuwa muwe wanyenyekevu , basi asifanye kiburi mmoja wenu kwa mwenziwe na wala mmoja wenu asijifakharishe kwa mwengine]]

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ ، أَقُوْلُ قَوِلِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الْكَرِيْمُ .

*** *** ***

اَلْحَمْدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ، وَلاَ عُدْوَانَ إِلاَّ عَلَى الظَّالِمِينَ . وَنَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ وَلِيُّ الصَّالِحِينَ ، وَنَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ إِمَامُ الأَنْبِيَاءِ وَالْمُرْسَلِينَ ، وَأَفْضَلُ خَلْقِ اللهِ أَجْمَعِينَ ، صَلَوَاتُ اللهِ وَسَلاَمُهُ عَلَيْهِ ، وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَالتَّابِعِينَ لَهُمْ بِإِحْسَانٍ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ :

Enyi waja wa ALLAH :

Ikiwa ihsani huzaa mapenzi baina ya aliyefanya ihsani na aliyefanyiwa,basi kwa hakika hakuna katika viumbe mwenye ihsani kubwa zaidi kwa wanaadamu kama bwana wa viumbe Muhammad (s.a.w),ni ihsani kubwa ambayo haiwezi kupatiwa malipo au shukrani muwafaka kwa viumbe,inatosha kutambua ya kuwa yeye mtume (s.a.w) ndiye aliyetuelekeza kwa Allah,tukamtambua na kumpwekesha,tukaelewa hakika ya uwepo wetu katika huu ulimwengu,na lengo la kuumbwa kwetu na kutambua mwisho wa maisha ya dunia,mtume (s.a.w) ametufundisha kukaa na watu,akatuelekeza katika tabia njema, basi nani anastahikia mapenzi zaidi katika viumbe kuliko mtume (s.a.w)?!,Ni wajibu wetu kumpenda mtume (s.a.w) na tupandikize mapenzi hayo katika nyoyo za watoto wetu,na mapenzi ya kweli kwa mtume wetu (s.a.w) huanzia moyoni kwa kumuheshimu na kumthamini zaidi kuliko kiumbe chochote,na tumpende kwa ndimi zetu kwa wingi wa kumsalia na kumuombea rehma kwa Allah,na kueneza mafundisho yake na kuinusuru sheria aliyokuja nayo,na tumpende kivitendo kwa kutekeleza yale aliyokuja nayo na kufuata sera zake na kujipamba na sunna zake ,hakika huko ndio kumpenda kihalisia bwana wa viumbe Muhammad (s.a.w),na huo ndio uhakika wa imani ya mja,kwani ametueleza mtume (s.a.w) katika hadithi:

"لا يؤمنُ أحدُكم حتى أكونَ أحبَّ إليه مِن والده وولده والناس أجمعين"

“Hatoamini mmoja wenu mpaka niwe mimi napendeza zaidi kwake yeye kuliko (hata) mzazi wake na watoto wake na watu wote”.

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاَةِ وَالسَّلاَمِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَاإِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى .

للهم أَعِزَّ الإسلامَ والمسلمين،وأَذِلَّ الشركَ والمشركين، ودَمِّرِ اللّهُمَّ جميعَ أعداءِ الحقِّ والدينِ .

"ربنا ءاتنا من لدنك رحمة وهيئ لنا من أمرنا رشدا".

اللهم استَخلِفْنَا في أرضِكَ كما استخلفتَ مَنْ قَبْلَنَا من عِبَادَك المؤْمنينَ، ومَكِّنْ لَنا دِينَنَا الذي ارتَضَيتَهُ لنا، وأَبْدِلْنَا بِخَوفِنَا أَمْنَا،وبِذُلِّنَا عِزّا،وبِفَقْرِنَا غِنًى، وبِتَشَتُّتِنَا وَحْدَةً، واجْمَعْنا عِلى كلمتك،وأَلِّفْ بين قُلوبِنا بطاعتك.

اللهم إِنَّا ضُعفاءُ فَقَوِّنَا، وإِنَّا أذلاءُ فأعِزَّنَا، وإنا فقراء فَأَغْنِنَا ، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام،وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خَلِّصِ المسجدَ الأقصى وسائرَ بِلادِ المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، وَاجْعَلْهاَ في أيدي عِبادِك المؤمنين،الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار".

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

مكانة صلاة الفجر

الحمدُ للهِ الذي جعلَ الصلاةَ كتابًا موقوتًا على المؤمنينَ، وأَلزمَ بها المسلمينَ فِيْ مُحكَمِ الذكرِ المبينِ، وأشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له،وأشهد أن محمدا عبدُه ورسولُه،خيرُ مَنْ صلَّى وصامَ وأدَّى المناسكَ العِظامَ، صلى الله عليه وعلى آله وصحبِه ومن اهتدَى بِهدْيِه واستنَّ بسنتِه وسار على نَهجِه إلى يومِ الدينِ.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ} آل عمران102

{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ

أَمَّا بَعْدُ: فَيَا عِبَادَ اللهِ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ علاَّمِ الغيوبِ، فإنها جسرُ النجاةِ من العذاب، والسبيلُ إلى نيلِ الثواب.

Ndugu waislamu:

Mcheni Allah mtukufu ,na mujuwe ya kuwa sala ni bora ya matendo yenu ya kiwili wili,na ni sababu ya kunyanyuliwa Daraja mbele ya mola wenu,na kupata furaha ya dunia na akhera,basi yule atakayeitunza sala ni wepesi kutunza matendo mengine,na yule atakayeipoteza ni wepesi kupoteza matendo mengine.

Ndugu waislamu:

Hakika katika sala zenye utukufu mkubwa katika uislamu ni sala ya alfajiri, ni yenye ujira na utukufu mkubwa,ingawa kuna watu wengi wanaipuuza sala hii,na imekuwa misikiti mingi ya waislamu inasikitikia uchache wa wanaosali alfajiri,basi ni wajibu kuhimizana katika kuitekeleza ibada hii tukufu.

Yamekuja maandiko mengi katika uislamu yanayohimiza kusali sala ya alfajiri,na kuonesha utukufu wake na umuhimu wake,kiasi ambacho Allah ameuapia wakati wa alfajiri,akasema :

﴿ وَٱلۡفَجۡرِ ۝١ ﴾ الفجر: ١

“Naapa kwa Alfajiri”

Kisha Allah akajaalia katika utukufu uliopo katika sala ya alfajiri ni kuhudhuriwa na Malaika watukufu, akasema:

﴿ أَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ لِدُلُوكِ ٱلشَّمۡسِ إِلَىٰ غَسَقِ ٱلَّيۡلِ وَقُرۡءَانَ ٱلۡفَجۡرِۖ إِنَّ قُرۡءَانَ ٱلۡفَجۡرِ كَانَ مَشۡهُودٗا ٧٨ ﴾
الإسراء: ٧٨

“Simamisha sala jua linapopinduka (likaenda magharibi) mpaka giza la usiku,na musiache qur-ani ya sala ya alfajiri,hakika qur-ani ya (sala ya) alfajiri inahudhuriwa na Malaika”.

Na katika hadithi aliyoipokea imam Rabiu bin Habib amesema mtume (s.a.w):

"تتعاقبُ فيكم ملائكةٌ بالليلِ وملائكةٌ بالنهارِ ،فيَجتمعونَ في صلاةِ الفجرِ، فتعرُجُ الملائكةُ الذينَ باتُوا فيكمْ فيسألهمْ ربُّهم وهو أعلمُ بِهِمْ، كيف تركتمْ عِبادي؟ فيقولونَ تركناهمْ وهم يُصلُّونَ وأتيناهمْ وهم يُصلُّونَ"

"Hupokezana zamu kwenu Malaika wa usiku na Malaika wa mchana,na hukutana wote wakati wa sala ya alfajiri,basi huondoka wale Malaika waliokuwa nanyi usiku,basi mola wao huwauliza naye akiwa ni mjuzi zaidi kwao,vipi mumewaacha waja wangu ? nao husema :” tumewaacha wakiwa wanasali na tuliwajia wakiwa wanasali”.

Na pia amesema mtume (s.a.w):

“Yule atakayesali sala ya isha katika jamaa,ni kama kasimama nusu ya usiku,na yule atakayesali sala ya asubuhi katika jamaa,ni kama amesimama usiku wote ”

Na sala ya alfajiri inakuweka katika ulinzi wa Allah,amesema mtume (s.a.w):

”من صلى الصُّبحَ فهو في ذِمَّةِ اللهِ“

“Yule atakayesali sala ya asubuhi basi atakuwa katika ulinzi wa Allah”

Basi jipe bishara njema ewe ambaye unadumisha kusali sala ya alfajiri kwa kupata fadhila hizi tukufu mbele ya mola wako,ama wewe unayepuuza sala hii na ukaizembea,sawa ikiwa huisali kabisa,au unaisali kwa kuichelewesha,au kila siku unakosa jamaa ,ni fadhila ngapi umezikosa pindi ulipoendekeza usingizi ukachelewa kusali!,na ni mema mangapi umeyakosa pindi ulipoipoteza sala ya alfajiri!,na ni khazina ngapi umezikosa pindi ulipofanya uvivu kutokana na sala ya alfajiri!.

Ndugu waumini:

Kwa upande wa pili ,yamekuja makemeo mengi yaliyo mazito kumhusu mtu anayepuuza sala ya alfajiri,miongoni mwa makemeo hayo ni hadithi ya mtume (s.a.w):

"إِنَّ أَثقلَ الصلاةِ على المنافقينَ صلاةُ العشاءِ وصلاةُ الفجرِ، ولو يَعلمونَ ما فيهمَا لَأَتوهُمَا وَلَوْ حَبْوًا"

"Hakika sala nzito juu ya wanafiki ni sala ya isha na sala ya alfajiri,na lau wangejua yaliyomo ndani yake (katika fadhila) wangekuja hata kwa kusota"

Basi je,unaridhika ndugu yangu kunasibishwa na wanafiki,na pia amesimulia Naafiu kutoka kwa sahaba Abdullah bin Omar (r.a) amesema:

"Tulikuwa sisi tunapomkosa mtu katika sala ya alfajiri humdhania vibaya"

فاتقوا الله عبادَ الله ! وتمسكوا بطاعته وداوموا على صلاة الفجر في المسجد لكي تفوزوا في الدنيا والآخرة.

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ، أَقُوْلُ قَولِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الْكَرِيْمُ.

*** *** ***

الحمدُ للهِ على إِحسانِهِ، والشكرُ له على توفيقِه وامتنانِه، وأشهد أن لا إله إلا الله وحدَه لا شريكَ له تعظيمًا لِشأنِه، وأشهد أن محمدا عبده ورسولُه الداعيْ إلى رِضوانِه، صلى الله وسلم عليه وعلى آله وصحبه أجمعين.
أما بعد:

Ndugu muislamu:

Tambua ya kuwa Allah kajaalia kila kitu na sababu yake,basi taka msaada kwa mola wako,na utafute sababu ambazo zitakusaidia kuhudhuria sala ya alfajiri,ikiwa utajitahidi na ukapigana na nafsi yako utaweza kuwa miongoni mwa wanaohudhuria sala hiyo,amesema Allah mtukufu:

﴿ وَٱلَّذِينَ جَٰهَدُواْ فِينَا لَنَهۡدِيَنَّهُمۡ سُبُلَنَاۚ وَإِنَّ ٱللَّهَ لَمَعَ ٱلۡمُحۡسِنِينَ ﴿٦٩﴾ ﴾ العنكبوت: ٦٩

"Na wale wanaojitahidi kwa ajili yetu tutawaongoza njia zetu,na kwa hakika Allah yuko Pamoja na watu wema".

Na miongoni mwa sababu zitakazokuwezesha kusali sala ya alfajiri kwa wakati wake,ni kulala mapema,haitakiwi kujishughulisha na mambo ya upuuzi baada ya sala ya isha,kwani alikuwa mtume (s.a.w) anachukia kulala kabla ya sala ya isha, na anachukia mazungumzo baada ya sala ya isha.

Na pia katika sababu hizo ni kulala kwa udhu,na kusoma dua za kulala zilizopokelewa kwa mtume (s.a.w),na kusoma ayatul kursy,na usome suratul Ikhlasi na Falaq na Annaas,na upanguse mwili wako, na ukariri hayo mara tatu,kisha ulale ubavu wako wa kulia,imekuja katika sahihul Bukhary ya" kuwa mtume (s.a.w) anapokaa kwenye kitanda chake kila usiku,hukusanya viganja vyake kisha hupuliza katika viganja hivyo,na husoma ndani yake suratul-ikhlas na suratul falaq,na suratunnaas,kisha hupangusa kwa viganja vyake juu ya kichwa chake na uso wake na sehemu zifuatazo katika mwili wake,anafanya hivyo mara tatu",na unaweza pia kuweka Alarm katika simu,na kutafuta sababu nyenginezo.

نسألُ اللهَ أن يُوفِّقَناَ لِطاعتِه ويُبلغَنَا مَرْضَاتِهِ، إنه وَلِيُّ ذلكَ والقادِرُ عليهِ.

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا:

{إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا}

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا.

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى. اللهم أَعِزَّ الإسلامَ والمسلمين، وأَذِلَّ الشركَ والمشركين، ودَمِّرِ اللّهُمَّ جميعَ أعداءِ الحقِّ والدينِ.

"ربنا ءاتنا من لدنك رحمة وهيئ لنا من أمرنا رشدا".

اللهم استخلِفْنَا في أرضِكَ كما استخلفتَ مَنْ قَبْلَنَا من عِبَادِكَ المُؤْمِنينَ، ومَكِّنْ لَنا دِينَنَا الذي ارتَضَيتَهُ لنا، وأَبْدِلْنَا بِخَوفِنَا أَمْنَا، وبِذُلِّنَا عِزّا، وبِفَقْرِنَا غِنًى، وبِتَشَتُّتِنَا وَحْدَةً، واجْمَعْنا عِلى كلمتك، وألِّفْ بين قُلوبِنا بطاعتك.

اللهم إنَّا ضُعفاءُ فَقَوِّنَا، وإنَّا أذلاءُ فأعِزَنَا، وإنا فقراء فَأَغْنِنَا، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام، وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خَلِّصِ المَسجدَ الأقصى وسائرَ بِلادِ المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، وَاجْعَلْهاَ في أيدي عِبادِك المؤمنين، الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار".

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ}.

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ

نعمة الزواج

الحمد لله الذي خلق من الماءِ بشَرًا فجعله نسبا وصِهْرًا، جعل الزواجَ مودةً ورحمةً وبِرًّا، وأشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريكَ له، له الأسماءُ الحسنى والصفاتُ العُلى، وأشهد أن سيدنا ونبينا محمدا عبده ورسوله أمرنا بالتمسك بالعروة الوُثْقَى،صلى الله وسلم عليه وعلى آله وصحبه والتابعين لهم بإحسان إلى يوم الدين.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ}

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ علاَّمِ الغيوبِ،فإنها جسرُ النجاةِ من العذاب، والسبيلُ إلى نيلِ الثواب .

Ndugu waislamu: Kwa hakika ni ihsani kubwa ambayo Allah ameifanya kwa waja wake kwa kuweka jambo tukufu la ndoa katika dini,na akalisisitiza na kuliwekea misingi imara ya kisheria,hakuna shaka ya kuwa ndoa ni neema kubwa isiyo na ukomo,ni vigumu kueleza yote katika kheri zake na manufaa yake,hebu tufikirie lau ingekuwa hakuna sheria ya ndoa namna uharibifu na ufisadi ungetawala katika jamii zetu,ingekosekana nidhamu,na lingeenea fujo na uovu,na maafa makubwa yasiyoelezeka.

Kwa ajili hiyo Allah mtukufu akaieleza ndoa katika qur-ani katika mtiririko wa neema nyingi ambazo amezineemesha kwa waja wake,akasema :

﴿ وَٱللَّهُ جَعَلَ لَكُم مِّنۡ أَنفُسِكُمۡ أَزۡوَٰجٗا وَجَعَلَ لَكُم مِّنۡ أَزۡوَٰجِكُم بَنِينَ وَحَفَدَةٗ وَرَزَقَكُم مِّنَ ٱلطَّيِّبَٰتِۚ ﴾

“ Na Allah amekuumbieni wake katika jinsi yenu na akakujaalieni kutoka katika wake zenu na akakuruzukuni vitu vizuri vizuri”

Ndugu waumini: Ukubwa wa neema hii tukufu unadhihirika katika faida nyingi zinazopatikana ndani yake,nazo ni nyingi mno miongoni mwazo ni :

1-KuwaNdoa ni sababu ya kujikinga kutokana na haramu,kuhifadhi tupu, na kuziepusha na starehe za haramu,kwa sababu mwanaadamu kaumbwa na matamanio na hisia ya kuvutika kwa jinsia nyengine,lau matamanio haya na hisia hisi zingepuuzwa katika dini basi jamii zingeharibika,na maadili yangeporomoka,na utu na tabia njema zingetoweka,na ndio maana mtume (s.a.w) akasema :

“يا معشر الشباب من استطاع منكم الباءة فليتزوج فإنه أغض للبصر وأحصن للفرج، ومن لم يستطع فعليه بالصوم فإنه له وِجاء".

“Enyi vijana,mwenye kumudu kati yenu majukumu ya ndoa basi aowe,kwani huko ni (sababu ya) kuinamisha macho kutokana na haramu,na kuhifadhi utupu,na Yule asiyeweza basi ajilazimishe kufunga kwani funga ni ngao kwake”.

2-Pia ndoa ni kihalalisho cha mume na mke katika starehe ya halali ,na kuweza kunufaika kila mmoja wao kwa mwengine kwa kupata haki zake,na mahitaji ya nafsi yake,mwanamme atamsimamia mkewe kwa kumpatia huduma zake za lazima,kama kula,kunywa,kivazi,na makaazi,na kumuelekeza katika yatayomnufaisha katika dunia na akhera,amesema ALLAH:

﴿ٱلرِّجَالُ قَوَّٰمُونَ عَلَى ٱلنِّسَآءِ بِمَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بَعۡضَهُمۡ عَلَىٰ بَعۡضٖ وَبِمَآ أَنفَقُواْ مِنۡ أَمۡوَٰلِهِمۡ

“ wanaume ni wasimamizi wa wanawake kwa kufadhiliwa na Allah baadhi yao juu ya baadhi na kwa mali zao wanazotoa”

Na mwanamke naye ataweza kumnufaisha mumewe katika haki za kutunza heshima yake na mali yake,na kulea watoto wake katika maadili mema,amesema Allah mtukufu:

فَٱلصَّٰلِحَٰتُ قَٰنِتَٰتٌ حَٰفِظَٰتٞ لِّلۡغَيۡبِ بِمَا حَفِظَ ٱللَّهُ

Basi wanawake wema ni wale ni wenye kutii na wanaoajilinda hata ktk siri kwa kuwa Allah ameamrisha wajilinde”

“”

3-Ndoa ni sababu ya kupatikana raha na utulivu wa nafsi,kiliwazo,na mapenzi yanayozaa matunda ya huruma na upole baina ya wanandoa,ndoa ni sitara ya kiwiliwili na utulivu wa nafsi,kwa kuwa mwanamke ndio tulizo la mwanamme huweza kujiliwaza kwake kutokana na dukuduku la huzuni na mihangaiko ya maisha,amesema Allah mtukufu:

﴿ وَمِنۡ ءَايَٰتِهِۦٓ أَنۡ خَلَقَ لَكُم مِّنۡ أَنفُسِكُمۡ أَزۡوَٰجٗا لِّتَسۡكُنُوٓاْ إِلَيۡهَا وَجَعَلَ بَيۡنَكُم مَّوَدَّةٗ وَرَحۡمَةً إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَأٓيَٰتٖ لِّقَوۡمٖ يَتَفَكَّرُونَ ﴾

“Na katika ishara zake kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao nae amejaalia mapenzi na huruma baina yenu hakika katika haya bila ya shaka zipo ishara kwa watu wanaofikiri “

4-Pia katika matunda ya ndoa ni kukaza kamba ya mahusiano mazuri baina ya jamii,na familia mbalimbali,kuna familia nyingi zilikuwa hazijuani,hazina ukaribu wowote,lakini ndoa ikaweza kuziunganisha familia hizo pamoja,zikawa zinaishi kwa umoja na ujamaa,ndio Allah akasema:

﴿ وَهُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ مِنَ ٱلْمَآءِ بَشَرًا فَجَعَلَهُۥ نَسَبًا وَصِهْرًا ۗ وَكَانَ رَبُّكَ قَدِيرًا ﴿٥٤﴾ ﴾ الفرقان: ٥٤

Nae ndie aliemuumba mwanaadamu kutokana na maji, akamjaalia kuwa na nasaba na ushemeji na Mola wako mlezi ni muweza".

5-Ndoa ni sababu ya kukithiri kwa umma wa mtume (s.a.w) ambapo mtume atakuja kujifakharisha siku ya kiama kwa wingi wa umma wake juu ya ummati nyengine, kama ilivyokuja katika hadithi ya Anas bin malik,aliyoipokea Ahmad na wengineo,amesema mtume (s.a.w) ;

"Oweni wanawake wenye mapenzi,na wenye kizazi,kwani kwa hakika mimi ni mwenye kujifakharisha kwa wingi wenu siku ya kiyama",ni lazima waislamu wakafanya pupa ya kutekeleza amri hii tukufu,na wakawawezesha vijana juu yake ili kuziokoa jamii kutokana na maradhi ya tabia mbaya,zinaa,liwati,udhalilishaji wa kijinsia,na hatimae kuenea watoto wa njee,na kuondoka amani na utulivu katika jamii zetu.

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ ، أَقُوْلُ قَولِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الْكَرِيْمُ .

***

الحمد لله رب العالمين، والعاقبة للمتقين، ولا عدوان إلا على الظالمين، وأشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له ولي الصالحين، وأشهد أن سيدنا ونبينا محمدا عبده ورسوله، صلوات الله وسلامه عليه وعلى آله وصحبه وعلى التابعين لهم بإحسان إلى يوم الدين.

أما بعد:

Ndugu waumini:Kwa hakika manufaa haya ya ndoa hayawezi kuleta athari zake kwa wanandoa na wanajamii kiujumla Ila kwa kufuata taratibu na adabu za kisheria katika kutekeleza jambo hili,kila kitu kinatakiwa kiendesahwe katika taratibu zake na mifumo yake,tukiangalia sasa hivi katika jamii zetu,tutakuta waowaji ni wengi,lakini wanaoudumu katika ndoa hizo kwa furaha na mapenzi na huruma ambayo Allah ameyataja katika qur-ani kuwa ndio natija ya ndoa ya kiislamu iliyo salama,ni wachache katika hao wanaoneemeka na kustarehe katika ndoa zao,kiukweli kadhia hii ni kubwa na ni nzito yahitaji maelezo mengi,na upekuzi zaidi kutoka kwa wataalamu,ila sababu kubwa ni kuyapuuza mafunzo ya dini,na kukiuka taratibu zake katika kutekeleza sharia hii,kuanzia utangulizi wake,na katika utekelezaji wake,lakini kwa wanandoa wenyewe pia kuna mengi yanayokosekana,ni wangapi wanaingia katika ndoa wakiwa hawana uwelewa wowote kuhusu hukumu ,haki , majukumu,na taratibu zake,ni muhimu haya yakazingatiwa na kupewa kipao mbele ,ili jamii zineemeke kwa neema hii,tumuombe Allah atuwezeshe kutekeleza amri zake,na kuwacha makatazo yake,na azitie Baraka ndoa zetu,na atupe kizazi chema kitakachosimama katika njia iliyo sawa.aamiin.

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَاإِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى . اللهم أَعِزَّ الإسلامَ والمسلمين،وأَذِلَّ الشركَ والمشركين، ودَمِّرِ اللّهُمَّ جميعَ أعداءِ الحقِّ والدينِ .

"ربنا ءاتنا من لدنك رحمة وهيئ لنا من أمرنا رشدا".

اللهم استخلِفْنَا في أرضِكَ كما استخلفتَ مَنْ قَبْلَنَا من عِبَادِكَ المُؤْمِنينَ، ومَكِّنْ لَنا دِينَنَا الذي ارتَضَيتَهُ لنا، وأَبْدِلْنَا بِخَوفِنَا أَمْنَا،وبِذُلِّنَا عِزّا،وبِفَقْرِنَا غِنًى، وبِتَشَتُّتِنَا وَحْدَةً، واجْمَعْنا عِلى كلمتك،وألِّفْ بين قُلوبِنا بطاعتك.

اللهم إنَّا ضُعفاءُ فَقَوِّنَا، وإنَّا أذلاءُ فأعِزَّنَا، وإنا فقراء فَأَغْنِنَا ، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام،وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خَلِّصِ المَسجدَ الأقصى وسائرَ بِلادِ المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، وَاجْعَلْهاَ في أيدي عِبادِك المؤمنين،الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار".

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

ولو كنت فظا غليظ القلب لا نفضوا من حولك

بسم الله الرّحمن الرّحيم .

الحَمْدُ للهِ مُبْدِعِ الْكَائِنَاتِ، وَبَارِئِ النَّسَمَاتِ، لَهُ الأَسْمَاءُ الْحُسْنَى ، وَعَظِيمُ النُّعُوتِ وَالصِّفَاتِ. أَحْمَدُهُ سُبْحَانَهُ بِمَا هُوَ لَهُ أَهْلٌ مِنَ الْحَمْدِ وَأُثْنِي عَلَيْهِ ، وَأَسْتَغْفِرُهُ مِنْ جَمِيعِ الذُّنُوبِ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ ، وَأُومِنُ بِهِ وَأَتَوَكَّلُ عَلَيهِ ، مَنْ يَهْدِهِ اللهُ فَلاَ مُضِلَّ لَهُ ، وَمَنْ يُضْلِلْ فَلاَ هَادِيَ لَهُ . وَأَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ ، قَيُّومُ الأَرْضِ وَالسَّمَاوَاتِ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ .وَأَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ ، بَلَّغَ الرِّسَالَةَ وَأَدَّى الأَمَانَةَ وَنَصَحَ الأُمَّةَ ، صَلَّى اللهُ عَلَيهِ وَسَلَّمَ وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ ، وَعَلَى كُلِّ مَنِ اهْتَدَى بِهَدْيِهِ وَاسْتَنَّ بِسُنَّتِهِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ.

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اتَّقُواْ اللّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ }آل عمران102

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلاً سَدِيداً * يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُم ويغفر لكم ذنوبكم ومن يطع الله ورسوله فقد فاز فوزا عظيما }

{ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ }

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عِبَادَ اللهِ ، أُوصِيْكُمْ وَنَفْسِي بِتَقْوَى اللهِ علاَّمِ الغيوبِ،فإنها جسرُ النجاةِ من العذاب، والسبيلُ إلى نيلِ الثواب .

Ndugu waislamu :

Upole na ustaarabu ni katika tabia zenye kuhimizwa katika dini yetu tukufu ,kwa kuwa ni tabia yenye kueneza mapenzi baina ya watu,na inamuweka karibu alie mbali, na ina hifadhi mapenzi kwa alie karibu , inampa faraja mwenye huzuni ,na kupunguza uzito wa tatizo na kuondoa gamu la nafsi , upole unamgeuza adui kua rafiki kipenzi , na mwenye chuki na hasira kua mstaarabu , na kumfanya bakhili kua mkarimu ,anakaa mwenye upole na watu mbali mbail hata wenye mioyo migumu , upole na ustaarabu ni silaha nyepesi , lakini ina nguvu kubwa na ina taathira ya ajabu katika nafsi za waja, ndio maana mitume ya ALLAH ikasifika na sifa ya upole , na bwana mtume Muhammad (s.a.w) akafika upeo mkubwa katika sifa hii tukufu , hadi mola mtukufu akamsifu kwa tabia hii , akasema ALLAH :

﴿ فَبِمَا رَحْمَةٍ مِّنَ ٱللَّهِ لِنتَ لَهُمْ ۖ وَلَوْ كُنتَ فَظًّا غَلِيظَ ٱلْقَلْبِ لَٱنفَضُّوا۟ مِنْ حَوْلِكَ ۖ ﴿١٥٩﴾ ﴾ آل عمران: ١٥٩

[[Basi ni kwa sababu ya rehma itokayo kwa Allah ndio umekuwa laini kwao,Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia.]]

Aya hii pamoja ya kuwa inaonyesha utukufu wa mtume Muhammad (s.a.w) ,lakini pia inatufunza ya kuwa msingi mkubwa wa kuweza kukaa na watu,na kuwaathiri kitabia na kuweza kuziteka nyoyo zao na kuingiza mapenzi katika nafsi zao ni kuwa na tabia ya upole,ulaini , ama kwa hakika upole huleta kheri kubwa,kutoka kwa jaabir bun abdil llah – radhi za ALLAH zimfikie – amesema :

Nimemsikia mtume anasema :

{{من يحرم الرفق يحرم الخيركله}}

[[Atakae nyimwa upole kwa hakika amenyimwa kheri zote]]

Ndugu waislamu :

Hakika njia nyepesi na ya haraka ya kufikia mtu malengo yake ni upole katika kauli na vitendo, hivyo ni kwa sababu upole ni tabia yenye kupendeza kwenye mioyo ya watu ,na pia huteka nafsi za watu kwa haraka , basi je ? hatuwi ni wapole ndugu waislamu ? na tukaacha Ugumu na hasira za ovyo, ambazo hazina sababu za msingi ? na tufuate muongozo wa mtume (s.a.w) usemao:

{{لا يكونُ الرفقُ في شيءٍ إلا زانَه ولا يُنزع من شيء إلا شانه}}

[[Upole hauwi katika jambo lolote isipokua utakipamba , na hauondoshwi upole katika jambo lolote isipokua utakichukiza]]

Mtume (s.a.w) ametahadharisha kutumia ghadhabu na ukali katika kuishi na watu, kwani hasira huondoa upendo na hutia uadui baina ya watu na inaifanya mioyo iwe na chuki na dhana mbaya , mwishoni huziba njia zote za uwezekano wa kufanikiwa unalo likusudia , hapo hutofaidika wewe wala kuwanufaisha wengine ,hakika kila kitu kina taratibu na sheria zake , anaetaka kufanya jambo kwa manufaa ya jamii na taifa kwa ujumla , lazima afate taratibu zake , na kutumia hikma na busara na upole zaidi katika maneno na vitendo, kwani waislamu walifanikiwa kuikomboa miji mbali mbali kwa sababu ya uungwana wao,ustaarabu na tabia njema za kuweza kuziteka nafsi za watu katika kuikubali dini ya uislamu , kwa hivyo tambueni ndugu waisilamu , mtu hawezi kufikiai malengo yake hata siku moja, kwa fujo na ukorofi na kukurupuka ,wala si kwa maneno mabaya na kejeli na kudharau watu, isipokua atafika pahala atakwama, nyuma amesha haribu na mbele amesha bomoa , anasema ALLAH mtukufu kuhusu Firauni na wachawi wake ambao walimkana na kumfuata nabii Musa (a.s) :

{{فَأُلْقِيَ السَّحَرَةُ سُجَّدًا قَالُوا آَمَنَّا بِرَبِّ هَارُونَ وَمُوسَى}}

[[wakaangushwa wanasujudu. Wakasema: Tumemuamini Mola Mlezi wa Harun na Musa! [70]]]

Akawatisha firaun kwa adhabu kali akisema :

{{قَالَ آَمَنْتُمْ لَهُ قَبْلَ أَنْ آَذَنَ لَكُمْ إِنَّهُ لَكَبِيرُكُمُ الَّذِي عَلَّمَكُمُ السِّحْرَ فَلَأُقَطِّعَنَّ أَيْدِيَكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ مِنْ خِلَافٍ وَلَأُصَلِّبَنَّكُمْ فِي جُذُوعِ النَّخْلِ وَلَتَعْلَمُنَّ أَيُّنَا أَشَدُّ عَذَابًا وَأَبْقَى}} [طه/71]

[[(Firauni) akasema: Oh! Mnamuamini kabla sijakupeni ruhusa? Hakika yeye ndiye mkubwa wenu aliye kufundisheni uchawi. Basi kwa yakini nitakukateni mikono yenu na miguu yenu kwa kutafautisha. Na nitakutundikeni misalabani katika vigogo vya mitende, na hapo kwa yakini mtajua ni nani katika sisi aliye mkali wa kuadhibu na kuiendeleza adhabu yake.]]

Likaja jawabu kwa haraka kwa kuonyesha kuridhika na itikadi mpya , :

{{قَالُوا لَنْ نُؤْثِرَكَ عَلَى مَا جَاءَنَا مِنَ الْبَيِّنَاتِ وَالَّذِي فَطَرَنَا فَاقْضِ مَا أَنْتَ قَاضٍ إِنَّمَا تَقْضِي هَذِهِ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا . إِنَّا آَمَنَّا بِرَبِّنَا لِيَغْفِرَ لَنَا خَطَايَانَا وَمَا أَكْرَهْتَنَا عَلَيْهِ مِنَ السِّحْرِ وَاللَّهُ خَيْرٌ وَأَبْقَى}} [طه/72-73]

[[Wakasema: Hatutokukhiari wewe kuliko ishara waziwazi zilizo tujia, na kuliko yule aliye tuumba. Basi hukumu utavyo hukumu; kwani wewe unahukumu haya ya maisha ya duniani tu. Hakika sisi tumemuamini Mola wetu Mlezi ili atusamehe makosa yetu na uchawi ulio tulazimisha kuufanya. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mbora na Mwenye kudumu zaidi.]]

Enyi waja wa ALLAH :

Luqmani amepigiwa mfano kwenye kitabu cha ALLAH , kwa kukaa na watoto wake vizuri na kuzungumza nao kwa hekima , akitaka kuwanasihi huwaita kwa majina mazuri yenye kuashiria upendo , upole,hayo yote ni kwa ajili ya kuonesha umuhimu wa kushikamana na tabia ya upole na hikma katika kuwanasihi watu,na kuwalingania katika tabia na maadili mema ,jambo hili linamhusu kila muislamu awe na nafasi yoyote ile katika jamii,awe ni mke ,mume , kaka , dada , mwalimu ,mwanafunzi , mlinganiaji ,shekhe, imamu khatwibu , mfanya biashara , na wote kwa ujumla , kwasababu kila mwanadamu hapa ulimwenguni , anapenda upole na anachukia ukali,Aly bin Abii Taalib anasema:(Mwenye kuwa mpole kwenye kusema amestahiki kupendwa).

فاتَّقُوا اللهَ– عِبَادَ اللهِ–وتَعَلَّمُوا مَا يَنْفَعُكُمْ فِي الدُّنْيَا وَالآخِرَةِ.

نَفَعَنِيَ اللهُ وَإِيَّاكُمْ بِهَدْيِ كِتَابِهِ ، أَقُوْلُ قَولِيْ هَذَا وَأَسْتَغْفِرُ اللهَ العَظِيْمَ لِيْ وَلَكُمْ ، فَاسْتَغْفِرُوهُ يَغْفِرْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيْمُ ، وَادْعُوهُ يَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّهُ هُوَ البَرُّ الْكَرِيْمُ .

*** *** ***

اَلْحَمْدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ، وَلاَ عُدْوَانَ إِلاَّ عَلَى الظَّالِمِينَ . وَنَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ وَلِيُّ الصَّالِحِينَ ، وَنَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا وَنَبِيَّنَا مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ إِمَامُ الأَنْبِيَاءِ وَالْمُرْسَلِينَ ، وَأَفْضَلُ خَلْقِ اللهِ أَجْمَعِينَ ، صَلَوَاتُ اللهِ وَسَلاَمُهُ عَلَيْهِ ، وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَالتَّابِعِينَ لَهُمْ بِإِحْسَانٍ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ .

أَمَّا بَعْدُ : فَيَا عَبَادَ اللهِ :

Enyi waja wa ALLAH :

Hakika Allah mtukufu amemtuma mtume wake Muhammad (s.a.w) ili aje kueneza upendo baina ya watu,ili aonyeshe namna ya kuishi na watu kwa upole na ustaarabu,na kueneza huruma katika ulimwengu, anamsifu mola wake akisema :

{{وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ}} [الأنبياء/107

[[Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.]]

Kwa sababu hio maisha yake yalikua yamejaa upole na huruma , hadithi aliyo ipokea Abuu huraira (r.a) amesema:" Siku moja alikuja bedui na akakojoa msikitini, maswahaba wakataka kumpiga na kumtoa nje ,mtume akasema kuwambia" mwacheni ,na mwagieni maji alipo kojolea ,kwani nimetumwa kuja kuwabashiria watu dini ya ALLAH sio kuwafukuza (na kuwachukiza)" , Anasi (R.A) pia anasimulia anasema;" Kuna mtu mmoja alikuja kwa mtume (s.a.w) wakati anatembea katika safari zake , akaja kumpiga begani mwake akimwambia , ewe Muhammad toa amri nipewe katika mali yako , mtume akamgeukia kisha akacheka kwa kutabasamu kisha akatoa amri ya kupewa anacho omba ", huyo ndio mtume wa ALLAH , tujitahidi kumuiga katika nyenendo zake , tupate mafanikio duniani na akhera ,

فتقوا الله عباد الله وتزينوا بالرفق , وتحلوا باللين ,وتقوا يوما ترجعون فيه إلى الله ثم توفى كل نفس ماكسبت و هم لايظلمون .

هَذَا وَصَلُّوا وَسَلِّمُوا عَلَى إِمَامِ الْمُرْسَلِينَ وَقَائِدِ الْغُرِّ الْمُحَجَّلِينَ ، فَقَدْ أَمَرَكُمُ اللهُ تَعَالَى بِالصَّلاةِ وَالسَّلامِ عَلَيهِ فِي مُحْكَمِ كِتَابِهِ حَيْثُ قَالَ عَزَّ قَائِلاً عَلِيْمًا :

{ إِنَّ اللهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا }

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَاإِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى سَيِّدِنَا إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلَ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ، وَارْضَ اللَّهُمَّ عَنْ خُلَفَاءِهِ الرَّاشِدِينَ وَعَنْ أَزْوَاجِهِ أُمَّهَاتِ الْمُؤْمِنِينَ ، وَعَنْ سَائِرِ الصَّحَابَةِ أَجْمَعِينَ ، وَعَنِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ إِلَى يَوْمِ الدِّيْنِ ، وَعَنَّا مَعَهُمْ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ.

اَللَّهُمَّ اجْعَلْ جَمْعَنَا هَذَا جَمْعًا مَرْحُومًا ، وَاجْعَلْ تَفَرُّقَنَا مِنْ بَعْدِهِ تَفَرُّقًا مَعْصُومًا ، وَلاَ تَدَعْ فِينَا وَلاَ مَعَنَا شَقِيًّا وَلاَ مَحْرُوْمًا .

اَللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى .

للهم أَعِزَّ الإسلامَ والمسلمين،وأَذِلَّ الشركَ والمشركين، ودَمِّرِ اللّهُمَّ جميعَ أعداءِ الحقِّ والدينِ .

"ربنا ءاتنا من لدنك رحمة وهيئ لنا من أمرنا رشدا".

اللهم استَخلِفْنَا في أرضِكَ كما استخلفتَ مَنْ قَبْلَنَا من عِبَادَك المُؤمِنينَ، ومَكِّنْ لَنا دِينَنَا الذي ارتَضَيتَهُ لنا، وأَبْدِلْنَا بِخَوفِنَا أَمْنَا،وبِذُلِّنَا عِزّا،وبِفَقْرِنَا غِنًى، وبِتَشَتُّتِنَا وَحْدَةً، واجْمَعْنا عِلى كلمتك،وألِّفْ بين قُلوبِنا بطاعتك.

اللهم إنَّا ضُعفاءُ فَقَوِّنَا، وإنَّا أذلاءُ فأعِزَّنَا، وإنا فقراء فَأَغْنِنَا ، اللهم أغننا بحلالك عن الحرام،وبطاعتك عن الآثام، وبك عمن سواك، يا الله ياذا الجلال والإكرام.

اللهم خَلِّصِ المَسجدَ الأقصى وسائرَ بِلادِ المسلمين من أرجاس القوم الكافرين، وَاجْعَلْهاَ في أيدي عِبادِك المؤمنين،الذين يقيمون الصلاة ويؤتون الزكاة ويأمرون بالمعروف وينهون عن المنكر.

"ربنا اغفر لنا ذنوبنا وكفر عنا سيئاتنا وتوفنا مع الأبرار".

"ربنا ظلمنا أنفسنا وإن لم تغفر لنا وترحمنا لنكونن من الخاسرين".

عباد الله:

{ إِنَّ اللهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَى وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ } .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .

اذْكُرُوا اللهَ الْجَلِيْلَ الكَرِيْمَ يَذْكُرْكُمْ ، وَاشْكُرُوهُ عَلَى نِعَمِهِ يَزِدْكُمْ ، وَلَذِكْرُ اللهِ أَكْبَرْ ، وَاللهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ .